JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

# SERA YA TAIFA YA MAENDELEO YA VIJANA YA MWAKA 2007

TOLEO LA MWAKA 2024

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

# SERA YA TAIFA YA MAENDELEO YA VIJANA YA MWAKA 2007

TOLEO LA MWAKA 2024

**JEDWALI LA YALIYOMO** .......... ii

**ORODHA YA VIFUPISHO** .......... v

**TAFSIRI YA MANENO** .......... vi

**DIBAJI** .......... viii

**SURA YA KWANZA** .......... 1

**UTANGULIZI NA HALI ILIVYO** .......... 1

1.1. Usuli .......... 1
1.1.1. Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) .......... 1
1.1.2. Mafanikio ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) .......... 2
1.1.3. Upungufu wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) .......... 2
1.1.4. Changamoto Katika Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) .......... 4
1.2. Hali Ilivyo .......... 5
1.2.1. Elimu na Ujuzi kwa Vijana .......... 5
1.2.2. Uvumbuzi na Ubunifu kwa Vijana .......... 6
1.2.3. Vijana na Mapinduzi ya Kidijitali .......... 7
1.2.4. Ajira kwa Vijana .......... 9
1.2.5. Ushiriki wa Vijana Katika Sekta za Kijamii na Kiuchumi .......... 11
1.2.6. Uzalendo, Kujitolea na Utaifa .......... 13
1.2.7. Afya na Lishe .......... 14
1.2.8. Malezi na Makuzi kwa Vijana .......... 15
1.2.9. Taaluma ya Maendeleo ya Vijana .......... 16
1.2.10. Uongozi na Utawala .......... 17
1.2.11. Masuala ya Vijana na Jinsia .......... 18
1.2.12. Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira .......... 19
1.2.13. Vijana Wenye Ulemavu .......... 20

**SURA YA PILI** .......... 23

**UMUHIMU WA SERA, DIRA, DHIMA NA MALENGO** .......... 23

2.1. Umuhimu wa Sera .......... 23
2.2. Dira .......... 23
2.3. Dhima .......... 42
2.4. Malengo ya Sera .......... 24

2.4.1. Lengo Kuu ... 24
2.4.2. Malengo Mahsusi ... 24

**SURA YA TATU ... 25**

**HOJA, MALENGO NA MATAMKO ... 25**

3.1. Elimu na Ujuzi kwa Vijana ... 25
3.2. Uvumbuzi na Ubunifu kwa Vijana ... 25
3.3. Vijana na Mapinduzi ya Kidijitali ... 26
3.4. Ajira kwa Vijana ... 27
3.5. Ushiriki wa Vijana Katika Sekta za Kijamii na Kiuchumi ... 28
3.6. Uzalendo, Kujitolea na Utaifa ... 28
3.7. Afya na Lishe ... 29
3.8. Malezi na Makuzi kwa Vijana ... 30
3.9. Taaluma ya Maendeleo ya Vijana ... 31
3.10. Uongozi na Utawala ... 31
3.11. Masuala ya Vijana na Jinsia ... 32
3.12. Vijana na Usimamizi wa Mazingira ... 33
3.13. Vijana Wenye Ulemavu ... 33

**SURA YA NNE ... 35**

**MFUMO WA KISHERIA ... 35**

**SURA YA TANO ... 36**

**MFUMO WA KITAASISI, UFUATILIAJI NA TATHMINI ... 36**

5.1. Mfumo wa Kitaasisi ... 36

5.2. Majukumu ya Wadau Katika Utekelezaji wa Sera ... 36
5.2.1. Wizara Yenye Dhamana na Maendeleo ya Vijana ... 36
5.2.2. Wizara Yenye Dhamana ya Masuala ya Fedha ... 36
5.2.3 Wizara Yenye Dhamana ya Masuala ya Mipango na Uwekezaji ... 37
5.2.4 Wizara Yenye Dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ... 37
5.2.5 Wizara Yenye Dhamana ya Kilimo, Uvuvi na Mifugo ... 37
5.2.6 Wizara Yenye Dhamana ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ... 37
5.2.7 Wizara Yenye Dhamana ya Masuala ya Afya ... 37
5.2.8 Wizara Yenye Dhamana ya Viwanda na Biashara ... 37
5.2.9 Wizara Yenye Dhamana ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ... 38
5.2.10 Wizara Yenye Dhamana na Usimamizi wa Mazingira ... 38
5.2.11 Wizara Yenye Dhamana ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ... 38

5.2.12 Wizara Yenye Dhamana na Mawasiliano na Teknolojia ya Habari .... 38
5.2.13 Wizara Nyingine za Kisekta, Idara na Wakala za Serikali .... 38
5.2.14 Mahakama .... 38
5.2.15 Sekretarieti za Mikoa .... 38
5.2.16 Mamlaka za Serikali za Mitaa .... 39
5.2.17 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania .... 39
5.2.18 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya .... 39
5.2.19 Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira .... 39
5.2.20 Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi .... 39
5.2.21 Ofisi ya Taifa ya Takwimu .... 39
5.2.22 Baraza la Vijana .... 39
5.2.23 Wazazi na Walezi .... 40
5.2.24 Familia na Jamii .... 40
5.2.25 Vijana .... 40
5.2.26 Asasi za Kiraia .... 40
5.2.27 Taasisi za Kitaaluma na Utafiti .... 40
5.2.28 Vyombo vya Habari .... 40
5.2.29 Wadau wa Maendeleo .... 40

5.3. Uratibu wa Utekelezaji wa Sera .... 41

5.4. Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini .... 41

5.5. Hitimisho .... 42

| | |
|---|---|
| **CAMARTEC** | Kituo cha Zana/Mitambo ya Kilimo na Teknolojia ya Vijijini |
| **FYDP** | Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano |
| **HBS** | Utafiti wa Hali ya Kipato cha Kaya |
| **HSHSP** | Mpango Mkakati wa Kudhibiti VVU na UKIMWI wa Sekta ya Afya |
| **ICTC** | Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **ILFS** | Utafiti wa Nguvu Kazi |
| **MAT** | Tiba Saidizi kwa Waraibu kwa Kutumia Dawa |
| **MKUHUMI** | Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa ya Ukaa Kutokana na Ukataji na Uharibifu wa Misitu |
| **MKURABITA** | Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania |
| **NEC** | Tume ya Taifa ya Uchaguzi |
| **NEEC** | Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi |
| **NGOs** | Mashirika Yasiyo ya Kiserikali |
| **SADC** | Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika |
| **SDGs** | Malengo Endelevu ya Maendeleo |
| **SIDA** | Shirika la Kimataifa la Ushirikiano wa Kimaendeleo la Sweden |
| **SIDO** | Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo |
| **SIGI** | Taasisi za Kijamii na Kielezo cha Jinsia |
| **SWM** | Sensa ya Watu na Makazi |
| **TDHS-MIS** | Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **TEMDO** | Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania |
| **TIRDO** | Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania |
| **UKIMWI** | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| **UNFPA** | Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani |
| **UNICEF** | Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto |
| **VVU** | Virusi vya Ukimwi |
| **WHMTH** | Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari |

| | |
|---|---|
| **Afya ya Uzazi** | Hali ya kuwa salama kimwili, kiakili, kijamii na katika mambo yote yanayohusiana na mfumo wa uzazi na utendaji wake wa kazi. |
| **Ajira** | Hujumuisha shughuli zinazokubalika kisheria, ambazo hufanyika ndani ya mipaka ya uzalishaji wa kitaifa, zenye staha na zinazozalisha kipato kwa kuzingatia kima cha chini cha mshahara wa sekta uliowekwa. |
| **Asasi Zinazoongozwa na Vijana** | Asasi za kiraia zilizoanzishwa na kusimamiwa na watu wenye umri wa miaka 15-35 kwa lengo la kutatua changamoto zinazowakabili. |
| **Hakimiliki** | Ni neno la kisheria linalohusisha haki inayotolewa kwa wabunifu katika kazi zao za uandishi na sanaa (ikiwa ni pamoja na programu za kompyuta). |
| **Hakimiliki Dhihini** | Mali iliyoko katika mfumo usioshikika kama vile kazi za ubunifu, ugunduzi, ishara na habari. Miliki dhihini ni tofauti na mali inayoshikika ambayo inatokana na ubunifu huo. Miliki Dhihini inatofautiana na vitu vinavyoshikika ambavyo inaambatana navyo. |
| **Hataza** | Haki ya kipekee iliyotolewa kwa ugunduzi katika eneo fulani kwa muda fulani, kwa ujumla wa miaka 20, baada ya kipindi hiki ugunduzi unapoteza umiliki wake na unaweza kutumiwa na mtu yeyote katika jamii. |
| **Jinsia** | Ni mahusiano ya kijamii na kiutamaduni yanayozingatia mgawanyo wa majukumu kwa kuangalia jinsi (Ke na Me). |
| **Kazi Zenye Staha** | Inajumuisha kazi zenye tija na malipo kwa jinsia zote zinazofanyika katika mazingira yanayolinda na kuzingatia haki za kazi, uhuru wa majadiliano, usalama mahali pa kazi, matarajio ya maendeleo binafsi, utu wa binadamu na ulinzi wa kijamii na familia. |
| **Kijana** | Kijana ni mtu mwenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi 35. |
| **Kujitolea** | Hali ya mtu, kundi la watu, au taasisi yoyote kutekeleza jambo au shughuli fulani kwa manufaa ya jamii bila ya kutarajia kupata malipo kutoka katika jamii au wale waliopata huduma. |
| **Pengo la Ujuzi** | Ujuzi alionao mtu kutokidhi mahitaji ya soko. |
| **Sekta Isiyo Rasmi** | Shughuli zisizo za kilimo, za kiwango kidogo na kujiajiri za kuzalisha mali katika kiwango cha chini, zenye mtaji mdogo na zitumiazo teknolojia ya kiwango cha chini. |

| | |
|---|---|
| **Sekta ya Sanaa** | Ni neno linalojumuisha sanaa, utamaduni, michezo na shughuli zingine za burudani. |
| **Sera** | Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana. |
| **Ubunifu** | Ubunifu ni mchakato wa kutafsiri wazo au ugunduzi kuwa bidhaa au huduma ambayo inajenga thamani ambayo wateja wanaweza kuwa tayari kugharimia. Inaweza kuwa katika mfumo wa bidhaa au huduma mpya au iliyoboreshwa, au kuwa katika mpangilio mpya au ulioboreshwa. |
| **Ujuzi** | Kiwango cha elimu na mafunzo ya ujuzi, maadili na utamaduni wa kufanya kazi. |
| **Ujuzi Kutolingana** | Tofauti kati ya ujuzi ambao mfanyakazi anao na ujuzi unaohitajika ili kutimiza jukumu kwa mafanikio. |
| **Ukatili wa Kijinsia** | Ni kitendo anachofanyiwa mtu yeyote mwanamke au mwanaume kwa lengo la kumdhuru au kumuumiza kisaikolojia, kimwili, kiafya, kingono na kiuchumi. |
| **Ukosefu wa Ajira** | Hali ya mtu kukosa kazi kabisa. Inaweza kuonekana kama hali ya kukaa bure kwa kulazimika, watu wenye uwezekanao wa kuzalisha kipato au kujiajiri ambao wana uwezo na wanataka kufanya kazi, lakini wameshindwa kupata kazi. |
| **Ushiriki wa Vijana** | Ushiriki wa vijana katika kubuni, kupanga na utekelezaji wa mipango, programu na miradi inayohusu maendeleo ya vijana na taifa kwa ujumla. |
| **Utaifa** | Hali ya mtu kuwa mzalendo, mwenye utii, uaminifu au utu kwa taifa lake. |
| **Uvumbuzi** | Ni matokeo au mchakato ambao hutoa njia mpya ya kufanya jambo au kutoa suluhisho jipya kwa tatizo la kiufundi. |
| **Uwezeshaji wa Vijana** | Ni mchakato ambao vijana wanawezeshwa na kuhimizwa kuyasimamia maisha yao. |
| **Uzalendo** | Hali ya mtu kuipenda, kuithamini na kujitolea kwa ajili ya nchi yake. |

Vijana wa Tanzania ni nguvu kazi kubwa yenye maarifa, uwezo na ubunifu na ndiyo wajenzi wa Taifa na ustawi na maendeleo endelevu. Kwa mujibu wa Utafiti wa Nguvu Kazi, 2021, Tanzania ina nguvu kazi ya watu 25,861,023 ambapo vijana ni 14,219,191 sawa na asilimia 55.6. Takwimu hizi zinadhihirisha kwamba, vijana ni nguvu kazi na rasilimaliwatu muhimu inayoweza kutumika kuleta mabadiliko chanya ya kisiasa, kijamii na kiuchumi nchini Tanzania.

Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007), Toleo la Mwaka 2024, inajengwa juu ya mafanikio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) ikiwa na lengo la kushughulikia mazingira yanayoendelea kubadilika ambayo vijana wa Tanzania wanakabiliana nayo. Kwa kutambua changamoto na fursa muhimu zinazoletwa na ulimwengu unaobadilika kwa kasi, Sera hii inaainisha mfumo kamili na madhubuti wa kuwawezesha na kuwaendeleza vijana kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Toleo hili linaendana na mabadiliko ya kidijitali, kuwawezesha vijana kuwa na ujuzi na maarifa stahiki ili kushiriki kikamilifu katika ulimwengu wa teknolojia. Aidha, Toleo hili linashughulikia masuala muhimu kama vile kushuka kwa maadili, changamoto za kiafya na lishe, na ufinyu wa fursa za uongozi kwa vijana. Sera hii pia inalenga kuwawezesha vijana wa Kitanzania kutumia uwezo na vipawa vyao kukuza na kuimarisha utamaduni wa uvumbuzi, ujasiriamali, uzalendo na utaifa.

Ifahamike kuwa, sera hii siyo juhudi ya mtu mmoja, bali ni mwongozo na ramani ya ushirikiano kati ya Serikali, mashirika ya kiraia, sekta binafsi na vijana ambao ni washiriki muhimu. Hivyo natumia fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa wote waliohusika katika uandaaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007), Toleo la Mwaka 2024. Shukrani za pekee ziende kwa watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) kwa kushiriki kikamilifu katika mchakato wa ukamilishaji wa Sera hii; Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA Tanzania); Shirika la Maendeleo la Canada; Shirika la Maendeleo la Sweden (SIDA) na Ubalozi wa Uswisi nchini Tanzania kwa misaada yao iliyowezesha kukamilika kwa sera hii.

Mwisho, nitoe wito kwa wadau wote wa masuala ya maendeleo ya vijana nchini, kutumia Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007), Toleo la Mwaka 2024 kama nyenzo na mwongozo muhimu katika utoaji wa huduma kwa vijana ili kujenga rasilimaliwatu muhimu kwa manufaa ya Taifa la Tanzania.

Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb)
**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu**
**(Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)**

## 1.1. Usuli

Vijana katika nchi yoyote duniani ni rasilimaliwatu muhimu kwa maendeleo na chachu ya mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia. Vilevile, ni rasilimali inayochangia maendeleo ya taifa na ni mtaji uliokusanywa wakati wa ujana balehe. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 (SWM 2022), Tanzania Bara ina jumla ya Watu 59,851,347. Kati ya hao, vijana ni 20,612,566 sawa na asilimia 34.4, ambapo wanaume ni 9,827,426 (16.4%) na wanawake ni 10,785,140 (18.0%). Aidha, vijana 12,312,403 wanaishi vijijini na 8,300,163 wanaishi mijini.

Vijana waliopo nchini ni kundi lenye mahitaji mbalimbali yanayoamuliwa na umri, jinsia, hali ya ndoa, viwango vya elimu, makazi na sifa nyinginezo za kijamii na kiuchumi. Kwa kuzingatia uwepo wa kundi kubwa la vijana lenye mahitaji mbalimbali, Serikali inatakiwa kuhakikisha kwamba vijana wote wanapata fursa sawa na kuwezeshwa kuwa raia wema, wenye kuwajibika, maadili na tija kwa jamii na Taifa.

Hivyo, kwa kutambua umuhimu wa vijana, Serikali imekuwa ikiandaa na kutekeleza sera, sheria, kanuni, miongozo na programu mbalimbali kwa lengo la kuwaendeleza na kuwawezesha vijana. Aidha, jitihada hizo zimekuwa zikitekelezwa kwa kushirikisha makundi yote ya vijana bila kujali jinsia, rangi, dini, mtizamo wa kisiasa na hali ya utimilifu wa kimwili na kiakili.

### 1.1.1. Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007)

Serikali katika kuhakikisha kwamba masuala ya maendeleo ya vijana yanapatiwa mwongozo na mwelekeo, imekuwa ikiandaa na kutekeleza sera mahsusi ya maendeleo ya vijana. Mwaka 1996, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya kwanza iliandaliwa, ambayo iliweka mfumo wa kisera wa kuwaendeleza na kuwawezesha vijana kwa kuwapatia huduma kwa ufanisi. Sera ya pili ya maendeleo ya vijana iliandaliwa na kuanza kutumika mwaka 2007 ili kuendana na mabadiliko mbalimbali ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiteknolojia yaliyojitokeza.

Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) ilikuwa na dira ya kuwa na vijana wenye uwezo, ari ya kutosha, kuwajibika na kushiriki kikamilifu katika nyanja zote za kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa maendeleo yao, jamii na taifa. Aidha, dhima yake ilikuwa ni kuweka mazingira yanayowezesha kujenga uwezo wa vijana, kukuza nafasi za ajira na kupata huduma za hifadhi ya jamii.

Lengo kuu la Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) lilikuwa kuwajengea uwezo, kuwawezesha na kuwaongoza vijana na wadau wengine katika utekelezaji wa masuala ya maendeleo ya vijana. Kadhalika, sera ilijielekeza mahsusi kuwawezesha vijana kupata ajira na uzoefu wa ajira na kukubali majukumu ili kuweza kuwa na mwenendo na maadili mema. Vilevile ilijielekeza kujenga mazingira yanayofaa kwa ajili ya vijana kushiriki katika kutoa maamuzi na kuongeza kasi ya kuanzisha

na kutumia huduma za kijamii zilizo rafiki kwa vijana. Vilevile, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) ililenga kutatua changamoto za huduma za afya kwa vijana; matumizi ya dawa za kulevya; uwezeshaji vijana kiuchumi; ushiriki wa vijana wakiwemo wenye ulemavu katika shughuli mbalimbali za maendeleo; ushiriki wa vijana kwenye masuala ya mazingira; usawa wa kijinsia na matumizi sahihi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

**1.1.2. Mafanikio ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007)**
Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) umekuwa na mafanikio mbalimbali ikiwemo kuongezeka kwa taasisi zisizo za kiserikali zinazojihusisha na masuala ya maendeleo ya vijana nchini kutoka 3,800 mwaka 2007 hadi 11,400 mwaka 2021 na kutungwa na/au kufanyiwa marekebisho kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura ya 410 na Kanuni zake za mwaka 2013 na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290. Aidha, mafanikio mengine ni kuanzishwa kwa kada ya Maendeleo ya Vijana katika ngazi ya mikoa na halmashauri ili kuratibu masuala ya vijana, na kuanzishwa kwa mafunzo ya Shahada ya Awali ya Utawala katika Maendeleo ya Vijana na Uongozi katika Chuo Kikuu Mzumbe.

Mafanikio mengine ni pamoja na kupungua kwa kiwango cha maambukizi ya VVU kutoka 2.15% mwaka 2011 hadi 0.66% mwaka 2021 kwa vijana wa umri wa miaka 15-19, na 5.55% mwaka 2011 hadi 1.0% mwaka 2023 kwa vijana wenye umri kati ya miaka 15-24; kupungua kwa kiwango cha mimba katika umri mdogo kutoka 24% mwaka 2010 hadi 22% mwaka 2022; kutengwa kwa ekari 274,091.33 za ardhi kwa ajili ya vijana kufanya shughuli za kiuchumi ambapo zaidi ya vijana 194,553 wamenufaika. Aidha Sera ilifanikisha uanzishwaji wa makampuni 345 ya vijana wajasiriamali mwaka 2022 kutoka makampuni 12 mwaka 2007; kuimarika kwa ushiriki wa vijana katika uongozi na tasnia ya utamaduni, sanaa na michezo; na kuimarika kwa ujumuishwaji wa vijana kwenye utekelezaji wa mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi ambazo zinawalenga vijana.

Kwa kuzingatia kuwa maendeleo ya vijana ni suala mtambuka, mafanikio haya yanatokana na utekelezaji wa sera, sheria, kanuni, miongozo na programu mbalimbali za kisekta zinazolenga kuwaendeleza na kuwawezesha vijana.

**1.1.3. Upungufu wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007)**
Taarifa ya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) iliyofanyika mwaka 2022 ilibaini kuwapo kwa upungufu katika utekelezaji wa sera kama ifuatavyo:

**(a) Baadhi ya Matamko ya Sera Kutojibu Hoja Zilizoainishwa**
Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) ina matamko ya sera ambayo hayajibu hoja zilizobainishwa. Baadhi ya matamko yenye upungufu huo yapo katika maeneo ya kisera yanayohusu fasili ya kijana; vijana na ushirikiano wa

kikanda na utandawazi; vijana, elimu na mafunzo; na haki za vijana. Upungufu huu unaweza kusababisha kuwekwa kwa jitihada ambazo hazitatui changamoto za vijana zilizokusudiwa na hivyo kushindwa kufikia malengo ya sera.

**(b) Dhima Kutoa Mwelekeo Usioendana na Dira ya Sera**

Uwepo wa dhima usiotoa mwelekeo wa namna ya kufikiwa kwa dira kunasababisha kutofikiwa kwa dira pamoja na malengo yaliyoainishwa kwenye mipango inayohusu maendeleo ya vijana kitaifa. Dhima ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) ilijielekeza kutatua changamoto za vijana kwenye maeneo yanayohusu ajira na hifadhi ya jamii pekee, wakati mwelekeo wa dira ulikuwa ni kutatuliwa kwa changamoto zilizoainishwa kwenye sera ili kuwa na vijana wenye uwezo, ari ya kutosha, kuwajibika na kushiriki kikamilifu katika nyanja zote za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

**(c) Sera Kutofafanua Kwa Kiasi cha Kutosha Baadhi ya Maeneo ya Msingi**

Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) haikutoa ufafanuzi wa kutosha katika baadhi ya maeneo ya msingi ikiwemo TEHAMA, elimu na mafunzo, huduma za afya, na ushiriki wa vijana na utawala bora hivyo kutoa mwanya wa tafsiri tofauti katika utekelezaji. Upungufu huu umesababisha changamoto katika utekelezaji ikiwa ni pamoja na wadau kukosa mwelekeo wa pamoja katika kushughulikia changamoto zinazowakabili vijana; kuwekwa kwa jitihada ambazo hazitatui changamoto zilizokusudiwa na uwezekano wa kutumia rasilimali katika shughuli ambazo hazichangii ipasavyo kufikia malengo ya sera. Aidha, sera haikuzingatia maeneo muhimu katika maendeleo ya vijana yakiwemo mapinduzi ya kidijitali; uzalendo na utaifa; umahiri na weledi katika sekta ya maendeleo ya vijana na mfumo madhubuti wa ushiriki, utambuzi na uendelezaji wa vijana wavumbuzi na wabunifu.

**(d) Sera Kutozingatia Baadhi ya Masuala Muhimu Yaliyoainishwa Kwenye Makubaliano na Itifaki Mbalimbali za Kikanda na Kimataifa**

Makubaliano na itifaki kuhusu maendeleo ya vijana zimeainisha masuala mbalimbali ambayo hayakuzingatiwa ipasavyo wakati wa kuandaliwa na kutekelezwa kwa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007).

Masuala hayo ni pamoja na ushiriki wa vijana katika mchakato wa kisiasa na ujenzi wa amani kwa ajili ya utulivu wa kisiasa, kijamii na kiuchumi kama ilivyobainishwa kwenye Ibara ya 8.1.5 ya Sera ya Vijana ya Afrika Mashariki (2013); Ibara ya 17 ya Mkataba wa Vijana wa Afrika (2006); Lengo Mahsusi Na. 5 la Mkakati wa Vijana wa Umoja wa Mataifa wa 2030 na Tamko la 4(13) la Agenda ya Afrika 2063; na utambuzi na uendelezaji wa vijana wavumbuzi na wabunifu kama ilivyo kwenye sehemu ya 3(b)(iii) ya Azimio la SADC Kuhusu Maendeleo na Uwezeshaji wa Vijana (2015).

Masuala mengine ni utambuzi wa taaluma ya maendeleo ya vijana na uanzishwaji wa programu za mafunzo husika katika elimu ya juu na vyuo vingine vya mafunzo kama ilivyofafanuliwa kwenye Ibara ya 11 ya Mkataba wa Vijana wa Afrika 2006; na lishe kwa vijana kama ilivyofafanuliwa kwenye Kipaumbele C cha Mpango Kazi wa Jumuiya ya Madola wa Uwezeshaji Vijana, 2015 na lengo Na. 2 la Malengo Endelevu ya Maendeleo 2030.

Kutozingatiwa kwa baadhi ya masuala yaliyobainishwa kwenye Mikataba, Itifaki na Makubaliano ya Kikanda na Kimataifa kunasababisha kutokuwapo kwa mikakati mahsusi ya kushughulikia masuala husika. Vilevile, kunasababisha upotevu wa imani na uaminifu kati ya nchi na wadau wengine wa kimataifa.

**(e) Kukosekana kwa Mkakati wa Utekelezaji**

Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) haikuwa na mkakati wa utekelezaji suala ambalo limesababisha kutokuwepo kwa ufanisi katika utekelezaji, uratibu na ufuatiliaji wa sera hiyo.

### 1.1.4. Changamoto Katika Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007)

Licha ya mafanikio yaliyopatikana, changamoto kadhaa zimeendelea kuwepo ikiwemo nguvu kazi kuwa na kiwango kidogo cha ujuzi wa juu na wa kati. Matokeo ya Utafiti wa Nguvu Kazi wa Mwaka 2021 yanaonesha kuwa 4.6% wana ujuzi wa juu ikilinganishwa na mahitaji ya 12%; 23.1% wana ujuzi wa kati ikilinganishwa na mahitaji ya 34%; na idadi kubwa kuwa na kiwango cha ujuzi wa chini sawa na 72.3% ikilinganishwa na 54% ya mahitaji.  Aidha, vijana wameendelea kukabiliwa na ukosefu wa ajira kwa kiwango cha 12.2% mwaka 2021; kupungua kwa kiwango cha ushiriki wa vijana katika kilimo kutoka 65.2% mwaka 2014 hadi 55.6% mwaka 2021 (ILFS, 2021) na ongezeko la vijana kwenye shughuli zisizo rasmi kutoka 10.1% mwaka 2006 hadi 59.9% mwaka 2022 (ILFS, 2006 na SWM, 2022).

Kadhalika, changamoto nyingine ni kutokutosheleza kwa huduma za afya ya uzazi kwa vijana; kuendelea kuwepo kwa changamoto ya mimba katika umri mdogo kwa kiwango cha 22% (TDHS-MIS, 2022); uratibu hafifu wa masuala ya maendeleo ya vijana katika sekta zote; na baadhi ya vijana kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya ambayo husababisha madhara mbalimbali ya kiafya, kijamii, kiuchumi, kimazingira na unyanyapaa. Aidha, changamoto ya usawa wa kijinsia miongoni mwa vijana katika maeneo mbalimbali kama vile ajira, elimu na umiliki wa rasilimali imeendelea kuwepo.

Kutokana na changamoto na upungufu wa kisera uliojitokeza, Taarifa ya Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Mwaka 2022 imeonesha msukumo wa kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007 ili kushughulikia upungufu na changamoto hizo. Tathmini pia imebaini umuhimu wa kuendelea na maeneo

yaliyoonesha mafanikio ambayo katika sera inayopendekezwa yatashughulikiwa kwa mtazamo tofauti unaoendana na mazingira ya sasa ili kuimarisha ustawi na maendeleo ya vijana nchini.

Vilevile, umuhimu wa kufanya mapitio ya sera hii umetokana na kuwepo kwa baadhi ya mipango ya Kikanda na Kimataifa ambayo Tanzania ni mwanachama. Mipango hii ni pamoja na Agenda ya Maendeleo ya Afrika (2063) inayosisitiza ushiriki wa watu wote kwenye ngazi za maamuzi; Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030) yanayosisitiza uwepo wa usawa katika makundi maalum wakiwemo vijana katika matumizi ya teknolojia mpya, kuongeza idadi ya vijana wenye ujuzi unaofaa na kupunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya vijana wasio katika ajira, elimu au mafunzo. Mipango mingine ni Sera ya Vijana ya Afrika Mashariki (2013) inayosisitiza ushiriki wa vijana kwenye masuala ya amani, ulinzi na usalama na Mkataba wa Vijana wa Afrika (2006) unaosisitiza nchi wanachama kuwa na sera ya taifa ya vijana inayojitosheleza.

### 1.2. Hali Ilivyo

Sehemu hii inafafanua hali ilivyo kwenye baadhi ya maeneo ya kisera ambayo yametokana na Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) iliyofanyika mwaka 2022. Maeneo haya ni pamoja na Elimu na Ujuzi; Uvumbuzi na Ubunifu; Vijana na Mapinduzi ya Kidijitali; Ajira; Ushiriki wa Vijana katika Sekta za Kijamii na Kiuchumi; Uzalendo, Moyo wa Kujitolea na Utaifa; Afya na Lishe, na Malezi na Makuzi ya Vijana. Maeneo mengine ni Taaluma ya Maendeleo ya Vijana; Uongozi na Utawala; Masuala ya Kijinsia; Vijana na Usimamizi wa Mazingira, na Vijana wenye Ulemavu.

Vilevile, sehemu hii inabainisha juhudi zilizofanyika, mafanikio yaliyopatikana, changamoto zilizopo na kupendekeza mwelekeo wa kisera ili kuwa na jamii yenye vijana wenye ujuzi, ubunifu, ufahamu na ujuzi wa teknolojia, waliowezeshwa, waliolelewa vyema, wazalendo na wawajibikaji.

#### 1.2.1. Elimu na Ujuzi kwa Vijana

Elimu bora inajumuisha maarifa na ujuzi unaoendana na mahitaji ya shughuli za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Elimu na ujuzi husika kwa vijana huongeza tija katika uzalishaji na utoaji wa huduma mbalimbali kwa jamii. Kadhalika, maendeleo ya kijana, pamoja na maendeleo ya jamii kwa ujumla, yana uhusiano usiotenganishwa na elimu bora na ujuzi unaoendana na mahitaji ya soko.

Katika kuwapatia elimu bora na ujuzi stahiki, Serikali kwa kushirikiana na wadau imekuwa ikitekeleza Mkakati wa Taifa wa Kukuza Ujuzi kupitia programu mbalimbali ili kuinua kiwango cha ujuzi wa nguvu kazi kukidhi mahitaji ya soko. Kupitia Mpango wa Kitaifa wa Kukuza Ujuzi, kwa wastani, vijana 42,407 katika soko la ajira hupatiwa ujuzi mbalimbali kwa mwaka kupitia programu za

uanagenzi, mafunzo kazini, na urasimishaji wa ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu. Jitihada nyingine ni pamoja na ukarabati na ujenzi wa vyuo vya mafunzo na ufundi stadi; uanzishwaji wa mitaala ya ujasiriamali katika vyuo vya elimu ya juu na kati kama vile Chuo cha Maendeleo ya Elimu ya Biashara, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo na taasisi nyingine na utekelezaji wa mpango wa elimu ya msingi na sekondari kwa wote bila malipo.

Licha ya juhudi zilizofanyika, Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) iliyofanyika mwaka 2022 imebaini kuwepo kwa vijana wenye ujuzi usioendana na mahitaji ya soko la ajira. Miongoni mwa sababu zinazochangia hali hii ni pamoja na taasisi za elimu ya juu kuzalisha idadi kubwa ya wataalamu ambao ni wasimamizi kuliko watendaji; uwepo wa mitaala ambayo haina uhusiano wa moja kwa moja na mahitaji ya soko la ajira, na vijana wengi wenye elimu ya msingi na sekondari kuingia kwenye soko la ajira bila ujuzi stahiki. Changamoto nyingine zilizobainika ni uwepo wa fursa finyu za mafunzo ya ufundi stadi hususan kwa vijana waliopo vijijini na uratibu hafifu wa mikakati na programu za ukuzaji ujuzi miongoni mwa vijana. Hali hii inasababishwa na mikakati na programu nyingi zilizopo kujikita zaidi mijini kuliko vijijini na uwepo wa wadau wanaotekeleza programu mbalimbali kwenye maeneo yanayofanana.

Ili kukabiliana na changamoto hizo, upo umuhimu wa kuwa na mwongozo wa kisera ambao ni mahsusi kwa vijana ili kuhakikisha nguvu kazi inapata ujuzi unaohitajika katika soko la ajira na kukuza ujuzi wa ujasiriamali, stadi za maisha na elimu ya kuendelea kujifunza miongoni mwa vijana.

#### 1.2.2. Uvumbuzi na Ubunifu kwa Vijana

Uvumbuzi na Ubunifu ni miongoni mwa vichocheo muhimu vya maendeleo ya vijana na uchumi kwa maendeleo endelevu. Kwa kuzingatia uwepo wa idadi kubwa ya vijana, suala la uvumbuzi na ubunifu linapaswa kupewa kipaumbele katika sera na mipango kwa maslahi mapana ya vijana na maendeleo ya taifa. Kwa msingi huo, serikali na wadau wana wajibu wa kuhakikisha kwamba, vijana wanawezeshwa kwa kupatiwa ujuzi stahiki wa uvumbuzi na ubunifu, kuibua vipaji, kushiriki kikamilifu katika elimu na uchumi unaoendeshwa na uvumbuzi na ubunifu ambao ndiyo msingi wa mapinduzi ya nne ya viwanda.

Wakati huo, Serikali imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya jinsi ya kuanzisha vituo vya ubunifu kwa taasisi za elimu ya juu ambayo yamewezesha kuanzishwa kwa kambi za ubunifu na atamizi kwa ajili ya uendelezaji uvumbuzi na ubunifu. Takwimu zinaonesha kwamba kuna jumla ya vituo atamizi 40 nchini ambavyo vipo katika mikoa ya Dar es Salaam (20), Mwanza (3), Mbeya (2), Dodoma (1), Lindi (1), Mtwara (1), Iringa (4), Arusha (6), na Kilimajaro (2). Takwimu hizi zinaonesha kuwa, mikoa 9 kati ya 26 ndiyo yenye vituo vya ubunifu na atamizi (Ripoti ya NEEC, 2023). Hii inaashiria uhaba wa miundombinu na fursa za uendelezaji wa masuala ya uvumbuzi

na ubunifu kwa vijana nchini. Kadhalika, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali kwa lengo la kuchochea ubunifu na ugunduzi nchini. Mathalani, kupitia mashindano ya Kimataifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, hadi kufikia mwaka 2023 zaidi ya wabunifu na wagunduzi 862 walitambuliwa. Kati yao, wabunifu mahiri 83 walitambuliwa na teknolojia 90 zilitambuliwa na kuhakikiwa. Bunifu hizo zinakusudiwa kuleta tija ya uzalishaji wa huduma katika sekta mbalimbali kama vile kilimo, maji, nishati, madini, afya, TEHAMA na elimu. Hata hivyo, mashindano hayo yamekuwa hayafanyiki mara kwa mara na yamejikita zaidi kwa vijana waliopo shuleni na vyuoni, hivyo kuwanyima fursa vijana walio nje ya mazingira ya shule na vyuo (Ripoti ya NEEC, 2023).

Aidha, taasisi za Serikali zilizopewa jukumu la kukuza uvumbuzi na ubunifu kama vile TIRDO, ICTC, COSTECH, TEMDO, SIDO, CAMARTEC na NEEC zinaendesha na kusaidia vijana katika maeneo ya mijini na kutoa fursa ndogo kwa wavumbuzi na wabunifu waliopo maeneo ya vijijini. Sambamba na changamoto hiyo, vijana wavumbuzi na wabunifu waliotambuliwa na taasisi hizo wanakabiliwa na ukosefu wa mitaji na usaidizi wa kitaalamu (Ripoti ya NEEC, 2023).

Vilevile, tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) iliyofanyika mwaka 2022 imebaini vijana kuwa mbali na taasisi za utafiti na maendeleo, ukosefu wa ujuzi wa kutosha kuhusu biashara ya uvumbuzi; matumizi madogo ya sayansi na teknolojia katika mfumo wa ubunifu wa msingi na uratibu usiotosheleza wa masuala ya uvumbuzi na ubunifu katika ngazi mbalimbali nchini.

Ili kukabiliana na changamoto hizo, kuna umuhimu wa kutoa mwongozo mahsusi wa kisera ambao utahakikisha matumizi sahihi ya sayansi na teknolojia katika kukuza uvumbuzi na ubunifu kwa vijana na kuongeza uelewa wa vijana juu ya aina tofauti za ubunifu na bunifu zilizopo. Aidha kuna haja ya kukuza na kuendeleza vipaji vya uvumbuzi na ubunifu kwa vijana na kuendeleza maeneo ya mfano ya biashara ili kukuza upatikanaji usiokuwa na vikwazo wa huduma za vituo atamizi na ubunifu.

### 1.2.3. Vijana na Mapinduzi ya Kidijitali

Mapinduzi ya kidijitali yanajumuisha anuwai ya sasa na inayokua kwa kasi ya teknolojia mpya kulingana na matumizi ya kidijitali ambayo yanaongeza ufanisi katika uzalishaji, huduma na mifumo ya utawala. Mapinduzi ya kidijitali ndiyo yanayoweka msingi wa kulipeleka taifa kwenye uchumi wa kidijitali unaowezeshwa na kuendeshwa na misingi muhimu ikiwemo TEHAMA na mifumo ya mawasiliano. Mapinduzi ya kidijitali kwa kiwango kikubwa yamebadilisha maisha ya vijana kutokana na matumizi ya intaneti na mifumo ya upatikanaji wa huduma hizo kama vile tarakilishi mpakato, vishikwambi na simu janja, pamoja na majukwaa ya mitandao ya kijamii na programu za kutuma ujumbe ambazo zimekuwa muhimu kwa maisha ya vijana ulimwenguni. Ripoti ya Hali ya Watoto Duniani ya Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF) 2017: Watoto katika Ulimwengu wa Kidijitali, inabainisha

kuwa mtumiaji mmoja kati ya watatu wa intaneti wana umri chini ya miaka 18. Vilevile, ripoti hiyo inabainisha kuwa, 71% ya vijana wenye umri wa miaka 15-24 wako mtandaoni, na kuwafanya kuwa kundi la umri lililounganishwa zaidi duniani kote. Kwa kuzingatia takwimu hizo, ufikivu wa teknolojia za kidigitali unawezesha vijana kutambua anuwai kamili ya haki zao za kiraia, kisiasa, kitamaduni, kiuchumi na kijamii.

Kwa kutambua umuhimu wa vijana na mapinduzi ya kidijitali, Serikali imechukua juhudi mbalimbali, ikiwemo uwekezaji katika miundombinu ya TEHAMA, ujenzi wa mkongo wa Taifa wa mawasiliano na kuweka mazingira wezeshi kwa wadau wengine kuwekeza katika sekta ya mawasiliano na utekelezaji wa mpango wa kufikisha mawasiliano vijijini na maeneo ya pembezoni ambapo Serikali inatarajia kusimika/kuboresha jumla ya minara 758 kwa teknolojia ya 3G/4G yenye brodibendi katika wilaya 127, kata 713, na vijiji 1,407. Serikali pia imeanzisha Mfuko wa Ufikivu wa Huduma ya Mawasiliano kwa Wote ili kuwezesha uwekezaji wa TEHAMA katika maeneo ya vijijini na mijini yenye upungufu wa huduma za mawasiliano (Taarifa ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ya Mwaka 2022).

Juhudi hizi zimechangia kuanzishwa kwa huduma za kifedha kwa njia ya simu nchini. Taarifa ya WHMTH, 2022 inabainisha kwamba, hadi kufikia Aprili, 2022, jumla ya laini za simu milioni 55.4 zilikuwa zimesajiliwa wakati watumiaji wa intaneti walikuwa milioni 29.9. Kadhalika, watumiaji wa huduma za kutuma na kupokea pesa kupitia mitandao ya simu walikuwa milioni 35.7.

Vilevile, uwepo wa mapinduzi ya kidijitali umewezesha upatikanaji wa ajira kwa vijana wengi kwenye masuala yanayohusu matumizi ya kidijitali kama vile uwakala wa huduma za kifedha kwa njia ya simu. Mafanikio mengine ni pamoja na kuunganishwa na mkongo wa Taifa kwa zaidi ya asilimia 45 ya watumiaji wa intaneti wakiwemo vijana; kuongezeka kwa idadi ya watoa huduma kwa kutumia njia za kisasa; na kuhama mfumo wa utangazaji kutoka analojia kwenda kidijitali (Taarifa ya WHMTH ya 2022).

Kiwango cha upatikanaji wa huduma za kidigitali ikiwemo TEHAMA kati ya kaya na watu binafsi inaonyesha kuwa, sekta hiyo inakua katika mwelekeo sahihi. Licha ya ukuaji huu, ushahidi kutoka kwenye Sensa ya Watu na Makazi, 2022 na taarifa za kiutawala inaonyesha kuwa pengo la mgawanyo wa kidigitali bado ni mkubwa. Kwa mfano, katika mtandao wa asilimia 72 ya kihamisha-data kasi, iliyotengwa kwa Tanzania, ni asilimia 45 tu inayotumika. Umiliki na matumizi ya vifaa vya TEHAMA (simu janja, vishikwambi na ngamiza) ni wa chini sana (19%), hivyo hupunguza matumizi ya huduma ya kihamisha–data kasi.

Vilevile, kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi, 2022, upatikanaji na matumizi ya huduma ya TEHAMA ni mdogo miongoni mwa wanawake ikilinganishwa na

wanaume katika maeneo ya mjini na vijijini; na umiliki na matumizi hafifu ya redio na runinga hudunisha mawasiliano ya habari na huduma muhimu. Hali hii inathibitishwa na kiwango cha umiliki na matumizi ya simu na vishikwambi, ambapo takribani asilimia 34 ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi wanaoishi mjini wanamiliki simu au vishikwambi ambapo kwa maeneo ya vijijini ni asilimia 9 tu.

Changamoto nyingine zilizobainishwa na taarifa ya tathmini ni pamoja na kuendelea kuwepo kwa matumizi yasiyo sahihi ya TEHAMA kwa vijana yanayosababisha vijana wengi kupoteza maadili na kujihusisha na wizi na udanganyifu wa kimtandao, na vijana kutokuwa na ujuzi wa kupima usalama na uaminifu wa maudhui mtandaoni. Vilevile, baadhi ya wazazi kutokuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu hatari ya matumizi mabaya ya TEHAMA kwa vijana, vijana kutoandaliwa vyema kutumia fursa au kunufaika na mapinduzi ya kidijitali kutokana na gharama kubwa ya vifaa na intaneti, ujuzi duni wa kidijitali na ufikivu hafifu wa mawasiliano ya intaneti katika maeneo ya vijijini.

Kutokana na uwepo wa changamoto hizo, kuna umuhimu wa kuwa na mwongozo mahsusi wa kisera ili kukuza ujumuishaji wa kidijitali kwa kutatua changamoto zinazohusiana na ufikivu, uwezo wa kumudu gharama za intaneti na ujuzi wa kidijitali miongoni mwa vijana. Hatua hii ni muhimu, siyo tu kwa sababu vijana ni kizazi kilichounganishwa zaidi, bali, wamethibitisha pasipo shaka kuwa wavumbuzi, watengenezaji wa suluhisho na watetezi imara kwa mustakabali bora na salama wa kidijitali.

**1.2.4. Ajira kwa Vijana**

Ajira ni nyenzo muhimu kwa maendeleo ya mtu binafsi, jamii na taifa kwa ujumla. Ajira humfanya mtu awe na ari ya kutosha, kuwajibika na kushiriki kikamilifu katika nyanja zote za kijamii na kiuchumi. Kwa mujibu wa Utafiti wa Nguvu Kazi, 2021 (ILFS, 2021), Tanzania, ilikuwa na nguvu kazi ya watu wapatao 25,861,023. Kati ya nguvu kazi hiyo, vijana ni 14,219,191 sawa na 55.6%. Aidha, kati ya nguvu kazi hiyo ya vijana, 6,950,530 ni wa kiume na 7,268,661 ni wa kike. Kati ya nguvu kazi ya vijana walioajiriwa ni 12,486,683 (wanaume 6,389,031 na wanawake 6,097,652) sawa na 87.8% ikilinganishwa na vijana 1,732,509 (Wanaume 561,500 na 1,171,009 wanawake) wasio na ajira.

Kadhalika, ILFS, 2021 inaonesha kuwa kiwango cha ushiriki wa vijana katika Nguvu Kazi kimepungua kutoka 84.5% mwaka 2014 hadi 80.3% mwaka 2021. Aidha, ushiriki wa nguvu kazi wa vijana katika maeneo ya vijijini ni 83.0% ikilinganishwa na 75.2% katika maeneo ya mijini. Pamoja na kupungua kwa kiwango cha ushiriki wa vijana katika nguvu kazi, vijana bado ni kundi kubwa ambalo linashiriki katika uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma katika soko la ajira. Kwa kutambua umuhimu wa ajira kwa vijana nchini, Serikali kwa kushirikiana na wadau inatekeleza sera, sheria, programu na miradi mbalimbali ili kuwawezesha vijana kujiajiri au kuajirika.

Sera, programu na miradi hiyo ni pamoja na utekelezaji wa programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora 2022-2030; Programu ya Ukuzaji Ujuzi ya mwaka 2015/2016-2025/2026; Sera ya Taifa ya Ajira ya Mwaka 2008; Sera ya Kilimo ya Taifa ya Mwaka 2013; Mpango wa Kitaifa wa Kukuza Ujuzi; Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati; Sheria ya Uwekezaji Tanzania Na. 10 ya Mwaka 2022; Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Sura ya 366; Sheria ya Kuratibu Ajira kwa Wageni Nchini Na.1 ya Mwaka 2015.

Licha ya juhudi zinazofanywa na serikali kukuza fursa za ajira, ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana ni suala linaloendelea kuwakabili kwa kuwa idadi kubwa huingia kwenye soko la ajira kila mwaka. Inakadiriwa kuwa takribani vijana 1,000,000 huingia sokoni kila mwaka huku 200,000 tu wakifanikiwa kupata ajira na 800,000 hawana uhakika wa ajira rasmi (FYDP III). Hali hii imepelekea kiwango cha ukosefu wa ajira kufikia 12.2% ambacho ni kikubwa kuliko lengo la taifa la kuwa na kiwango cha 8% (FYDP III). Changamoto ya ukosefu wa ajira ni kubwa kwa vijana wa kike (16.1%) kuliko wa kiume (8.1%). Aidha, ukosefu wa ajira ni mkubwa katika maeneo ya mijini kwani imefikia 13.7% ikilinganishwa na vijijini ambayo ni 9.8%. (ILFS, 2021). Ukosefu wa ajira una athari kubwa kwa mtu binafsi na familia. Ukosefu wa ajira husababisha ugumu wa maisha kutokana na ukosefu wa fedha, vile vile watu wasio na ajira wanaweza kuhisi kutengwa na jamii na kukosa kujiamini.

Aidha, ILFS (2021) inaonesha kuwa takribani 80.1% ya vijana walio katika ajira Tanzania Bara wako katika mazingira hatarishi ya ajira, ambapo wanawake wako katika mazingira hatarishi zaidi kuliko wanaume. Kiwango hicho kinaashiria kwamba, vijana walio katika mazingira hatarishi ya ajira hawana huduma za kinga ya jamii ambazo ni muhimu wakati wa majanga kama vile ulemavu, hali ya umaskini na nyakati za changamoto za kiuchumi. Vilevile, baadhi ya vijana wanafanya kazi pasipokuwa na mikataba au uelewa wa maudhui ya mikataba waliyonayo, na wengine hawafahamu haki zao kwa mujibu wa sheria za kazi na ajira.

Hivyo, kwa kuzingatia changamoto hizo, kuna umuhimu wa kuwa na mwongozo mahsusi wa kisera ili kutatua changamoto zinazohusiana na ajira kwa vijana, ikiwemo ukosefu wa ajira. Mwongozo huo ni pamoja na kuweka/kuhakikisha mazingira wezeshi ya kiuchumi ili kuvutia uwekezaji wa ndani na nje ya nchi katika maeneo yenye fursa za kutoa ajira mfano viwanda vya kutengeneza bidhaa; kuimarisha mazingira wezeshi, kukuza na kuvutia sekta binafsi na wadau wengine wa ajira kuelekeza uwekezaji kwenye sekta zenye kuajiri watu wengi; kuimarisha tafiti kuhusu ujuzi katika soko la ajira ili kuendeleza mafanikio yaliyofikiwa katika ajira; kuongeza upatikanaji wa elimu na mafunzo ya amali, kukuza ujasiriamali na kujiajiri, pamoja na kuimarisha uhusiano kati ya waajiri, wanaotafuta ajira, na taasisi za mafunzo; na kuhakikisha upatikanaji wa taarifa za soko la ajira zinazotosheleza mahitaji ya mipango na maamuzi.

### 1.2.5. Ushiriki wa Vijana Katika Sekta za Kijamii na Kiuchumi

Ushiriki wa vijana katika sekta za kijamii na kiuchumi unahusisha uwezo wa vijana kumiliki, kuongoza, kusimamia na kuendesha shughuli mbalimbali za kimaendeleo katika sekta za kijamii na kiuchumi kwa manufaa yao na taifa. Kwa muktadha wa sera hii, sekta za kijamii na kiuchumi ni pamoja na kilimo; nishati na madini; huduma za utalii na ukarimu; shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi na kifedha; usafiri na usafirishaji; sekta isiyo rasmi; viwanda na ujenzi; tasnia ya utamaduni, sanaa na michezo, na TEHAMA.

Kwa mujibu wa utafti wa nguvu kazi wa mwaka 2021, sekta hizi ni miongoni mwa sekta ambazo hushirikisha idadi kubwa ya vijana katika kujipatia kipato. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeweka mifumo mbalimbali ya kisera, kisheria, programu, mikakati na miongozo mbalimbali kwa lengo la kukuza na kuimarisha ushiriki wa vijana katika sekta hizo. Uchambuzi wa ushiriki wa vijana katika sekta hizo umefafanuliwa kwenye maeneo yafuatayo:

**Sekta ya Kilimo:** Sekta ya kilimo imeendelea kuwa chanzo kikuu cha ajira kwa vijana na inachangia takribani 26.2% ya Pato la Taifa la Tanzania (Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa, 2022). Hata hivyo, takwimu zinaonesha kuwa, ushiriki wa vijana katika kilimo umepungua kutoka 65.2% mwaka 2014 hadi 55.6% mwaka 2021 (ILFS, 2021). Kupungua huku kunaweza kuwa kumesababishwa na kuwepo kwa mifumo duni na fursa chache katika upatikanaji wa mitaji, ardhi, masoko na huduma za ushauri; utayari mdogo wa vijana kushiriki katika shughuli za vijana; kilimo kuendelea kuwa cha kutegemea mvua; kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi vijijini na miundombinu isiyo rafiki kwa maendeleo ya kilimo.

**Sekta Isiyo Rasmi:** Sekta isiyo rasmi imeendelea kuwa muhimu kwa kutoa ajira miongoni mwa vijana. Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kwa lengo la kupunguza ukubwa wa sekta hii ili kuwawezesha vijana kuendesha shughuli za kiuchumi na kumiliki rasilimali katika sekta rasmi. Jitihada hizo ni pamoja na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ili vijana wanaomiliki rasilimali na shughuli za kiuchumi katika sekta isiyo rasmi waweze kuzirasimisha (Ripoti ya Tathmini ya Sekta Isiyo Rasmi Tanzania, 2018). Aidha ripoti hii inabainisha kuwa, pamoja na sekta hii kuchukua vijana wengi, bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo uhaba wa maeneo ya kudumu ya kufanyia biashara; uhakika wa masoko, mikopo na taarifa muhimu za biashara; ujuzi unaohitajika na soko la ajira na matumizi ya teknolojia.

Pamoja na jitihada hizo, kumekuwa na ugumu wa vijana kuhitimu na kuelekea kwenye shughuli zilizopo kwenye sekta rasmi. Hali hii imethibitishwa na kuongezeka kwa kiwango cha ushiriki wa vijana katika sekta isiyo rasmi kutoka 10.1% mwaka 2006 hadi 59.9% mwaka 2022 (SWM 2022). Takwimu hizi zinaashiria kuwa, vijana wengi wanaendesha shughuli za kiuchumi na kumiliki rasilimali nje ya mfumo rasmi

na wanazidi kuongezeka kufanya kazi kwenye mazingira magumu na hatarishi (ILFS, 2021).

**Sekta ya Utamaduni, Sanaa na Michezo:** Sekta hii ni moja ya sekta zinazokua kwa kasi nchini. Shughuli za sekta hii zinajumuisha maigizo, muziki, na uendeshaji wa tovuti za makumbusho, michezo ya bahati nasibu, michezo mbalimbali na shughuli za burudani. Kwa mujibu wa Ripoti ya Hali ya Uchumi wa Tanzania kwa Mwaka 2022 sekta ya utamaduni, sanaa na michezo huchangia 0.4% ya Pato la Taifa kila mwaka. Kwa upekee, sekta hii ilichangia takriban trilioni 1.1 mwaka 2020 ikilinganishwa na bilioni 71 mwaka 2007.

Aidha, utafiti wa Nguvu Kazi wa Mwaka 2021 umebaini kuwa, ushiriki wa vijana katika sekta ya utamaduni, sanaa na michezo ni 0.2% ikiashiria ushiriki mdogo wa vijana. Hali hii inatokana na ukosefu wa mikakati maalumu inayowezesha vijana kushiriki kikamilifu katika sekta hii. Vilevile, Tathmini ya Sera ya Maendeleo ya Vijana (2007) ilibaini kuwa, changamoto zilizoainishwa wakati wa kutungwa kwa sera hiyo bado zimeendelea kuwepo, hivyo kuhitaji mtazamo na mwelekeo mpya wa kisera ili kuzitatua.

**Sekta Nyingine Muhimu:** Utafiti wa Nguvu kazi wa Mwaka 2021 unaonesha viwango tofauti vya ushiriki wa vijana katika sekta nyingine muhimu za kijamii na kiuchumi. Mathalani, ushiriki wa vijana katika biashara za jumla na rejareja, ukarabati wa magari na pikipiki (12.5%); viwanda (4.9%); uchukuzi (3.5%); madini na nishati (1.0%); shughuli za malazi na huduma za chakula (3.0%); ujenzi (2.6%); shughuli nyingine za huduma (1.9%) na shughuli za fedha na bima (0.4%). Takwimu hizi zinaashiria kuwa, kuna ushiriki hafifu wa vijana katika umiliki, usimamizi, na uendeshaji kwenye sekta hizo muhimu za kijamii na kiuchumi.

Miongoni mwa sababu zilizopelekea ushiriki hafifu wa vijana kwenye sekta muhimu ni pamoja na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) kukosa matamko mahsusi ya kisera ambayo yangewezesha kuandaliwa kwa mikakati na programu kwenye sekta hizo. Vilevile, sera haikufafanua wala kutambua ushiriki wa vijana wanaoishi nje ya nchi kwenye masuala ya kijamii na kiuchumi, hivyo kutojumuishwa ipasavyo katika uchumi wa nchi.

Ili kukabiliana na changamoto hizo, kuna umuhimu wa kukuza na kuimarisha ushiriki wa vijana katika sekta za kijamii na kiuchumi kwa kuhakikisha upatikanaji wa mitaji, masoko na huduma za ushauri kwa vijana; kuwa na mifumo rafiki ya uanzishwaji na uendelezaji wa biashara kwa vijana; uwepo wa mifumo madhubuti ya urasimishaji wa sekta isiyo rasmi; na kukuza ubia wa biashara ulioanzishwa na kusimamiwa na vijana.

#### 1.2.6. Uzalendo, Kujitolea na Utaifa

Uzalendo ni hali ya mtu kuipenda, kuithamini, kujitoa na ikibidi kuifia nchi yake. Aidha, kujitolea ni hali ya mtu, kundi la watu, au taasisi yoyote kutekeleza jambo au shughuli fulani kwa manufaa ya jamii bila ya kutarajia malipo kutoka kwenye jamii au wale waliopata huduma. Kwa upande mwingine, utaifa ni hali ya mtu kuwa mzalendo na mwenye utii, uaminifu na utu kwa Taifa lake. Hivyo, vijana wenye uzalendo, ni hazina kubwa katika kukuza umoja, mshikamano, amani, usalama na utulivu wa kisiasa na kiuchumi nchini.

Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kukuza na kuimarisha uzalendo kwa vijana, zikiwemo utekelezaji wa programu ya mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa yenye lengo la kuwapa vijana mafunzo ya awali ya kijeshi na stadi za kazi ili kuwajengea ukakamavu, uzalendo, umoja wa kitaifa na uwezo wa kujitegemea. Hata hivyo, Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) iliyofanyika mwaka 2022 imebaini kuwa, utekelezaji wa programu hii umekuwa ukikabiliwa na changamoto mbalimbali kuchukua idadi ndogo ya vijana ikilinganishwa na mahitaji.

Aidha, Serikali imeendelea kutoa elimu ya uraia na kuratibu wiki ya vijana na kambi za kitaifa kwa lengo la kukuza uzalendo na moyo wa kujitolea nchini. Hata hivyo, juhudi hizi zimekuwa zikihusisha idadi ndogo ya vijana, na hivyo kufanya elimu ya uraia na kujitolea kuwafikia wachache. Jitihada nyingine ni pamoja na mbio za Mwenge wa Uhuru; matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye vyombo vya habari, tamthilia na nyimbo za kizalendo na ushairi; ngoma za asili; mitandao ya kijamii; utoaji wa mafunzo ya mgambo na skauti; na matumizi ya alama za Taifa kama vile Ngao ya Taifa, Wimbo wa Taifa na Bendera ya Taifa.

Hata hivyo, pamoja na kuwepo kwa jitihada hizi, hali ya uzalendo, kujitolea na utaifa miongoni mwa vijana imeendelea kudorora kutokana na mifumo iliyokuwa inatumika kupandikiza vitu hivyo kutokuwa na ufanisi kwa sababu ya mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia. Hali hii imesababisha mmomonyoko wa maadili miongoni mwa vijana na kusababisha kuongezeka kwa uhalifu, uharibifu wa mali na ukosefu wa usalama wa mali na raia. Athari nyingine ni vijana kutokuwa na moyo wa kujitolea katika shughuli za ujenzi wa Taifa na masuala mbalimbali ya huduma za jamii.

Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) iliyofanyika mwaka 2022 imebaini kuwa, sera hii haikuwa na tamko mahsusi kwa ajili ya kuwezesha uwepo wa mikakati ya kukuza na kuimarisha uzalendo na utaifa kwa vijana. Hivyo, kutokana na changamoto hizo, kuna umuhimu wa kuwa na mwongozo mahsusi wa kisera ili kuimarisha mifumo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa itakayoimarisha uzalendo, utaifa na moyo wa kujitolea kwa vijana.

### 1.2.7. Afya na Lishe

Afya na lishe ni masuala ya msingi na mtambuka ambayo yana mchango mkubwa katika ustawi wa vijana kwa kuwa huwawezesha kushiriki katika shughuli za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kwa kutambua umuhimu wa masuala haya kwa vijana, Serikali imeendelea kubuni na kutekeleza sera, sheria, programu, mkakati na miongozo mbalimbali kwa lengo la kuwa na vijana wenye afya bora.

Miongoni mwa mipango hiyo ni pamoja na Mpango Mkakati wa Kudhibiti VVU na UKIMWI wa Sekta ya Afya (HSHSP IV) 2017- 2022; Programu ya Mama Wadogo, Stadi za Maisha na Afya ya Uzazi; Mpango Kazi wa Taifa wa Lishe wa Sekta Mbalimbali 2021/22 – 2025/26; Mpango Kazi wa Wizara ya Kilimo kuhusu Masuala ya Lishe 2021/22 – 2025/26; Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya Mwaka 2015; na Sera ya Taifa ya Afya (2007). Juhudi nyingine ni uboreshaji wa miundombinu ya afya; uanzishwaji wa Kamati ya Uongozi Ngazi ya Kitaifa kuhusu masuala ya lishe, na utekelezaji wa programu za lishe shuleni.

Hata hivyo, katika miongozo na programu hizo, vijana wanachukuliwa kama sehemu ndogo ya walengwa badala ya kuwa walengwa wakuu wanaohitaji uangalizi maalum, msaada, matunzo na huduma.

Licha ya mafanikio yaliyopatikana, vijana wameendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali za kiafya ikiwemo afya ya uzazi ambapo takwimu zinaonesha kuwa, mimba katika umri mdogo zimeendelea kuwepo kwa kiwango cha 22% mwaka 2022. Hivyo, ni muhimu kuhakikisha kuwa wasichana wanapata fursa za kuendelea na masomo na kupata ujuzi wa kuwawezesha kupata ajira zinazostahili (Taarifa ya SIGI, Tanzania, 2022).

Vilevile, Utafiti wa Viashira na Matokeo ya UKIMWI Tanzania, 2022/2023 umebaini kuwa, kiwango cha maambukizi ya VVU kwa vijana kipo juu zaidi kwa wanawake (0.8%) kuliko wanaume (0.3%) kwa vijana wa miaka 15-19; 1.8% (wanawake) ikilinganishwa na 0.9% (wanaume) kwa vijana wenye umri wa miaka 20-24; 3.2% (wanawake) ikilinganishwa na 1.8% (wanaume) kwa vijana wa miaka 25-29 na 6.6% (wanawake) ikilinganishwa na 2.1% (wanaume) kwa vijana wenye umri wa miaka 30-34. Takwimu hizi zinaashiria kwamba, vijana hususani wasichana wanakabiliwa na hatari ya magonjwa ya zinaa zaidi kuliko wavulana. Aidha, Tathmini ya Utekelezaji wa Sera (2007) imebaini kuwa, kiwango kidogo cha maambukizi kwa vijana wa kiume kinatokana na tabia ya kutojitokeza kupima VVU na kutegemea majibu kutoka kwa wenza wao.

Aidha, Serikali imeendelea kupambana na tatizo la uzalishaji, matumizi na biashara ya dawa za kulevya nchini. Hata hivyo, tatizo la matumizi ya dawa za kulevya kwa vijana limeendelea kuwepo pamoja na juhudi za udhibiti zinazofanywa na Serikali. Hali hii inadhihirishwa na watumiaji wanaojitokeza kutafuta tiba katika vitengo vya

afya ya akili kwenye hospitali za wilaya, mkoa na rufaa, nyumba za upataji nafuu, vituo vinavyotoa tiba saidizi kwa waraibu kwa kutumia dawa (MAT) na asasi za kiraia. Ingawa hakuna takwimu halisi ya vijana watumiaji wa dawa za kulevya nchini, waraibu 905,902 walijitokeza kupata tiba ya uraibu wa dawa mbalimbali za kulevya nchini kwa mwaka 2021 (DCEA, 2021). Matumizi ya dawa za kulevya yana athari mbalimbali za kiafya, kijamii, kiuchumi, kimazingira na unyanyapaa.

Vilevile, Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) iliyofanyika mwaka 2022 ilibaini kuwa, vijana wengi wanakabiliwa na magonjwa yasiyo ya kuambukiza na upungufu wa virutubishi muhimu mwilini. Hali hii inasababisha wengi wao kushindwa kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kijamii na kiuchumi na wengine kukabiliwa na athari mbaya katika mfumo wa afya ya uzazi. Magonjwa yasiyo ya kuambukiza ni mtambuka kwa kuwa ni 25% pekee yanatibiwa kwa kutumia afua za afya na 75% nje ya sekta ya afya. Aidha, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) haikuwa na matamko ya kisera yanayohusiana na kukabiliana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza na upungufu wa virutubishi muhimu mwilini kwa vijana.

Kwa kutambua changamoto hizo, upo umuhimu wa kuwa na mwongozo mahsusi wa kisera ambao utahakikisha uwepo wa mifumo jumuishi ya afya; udhibiti wa dawa za kulevya na uimarishaji wa afya ya uzazi kwa vijana; kukuza afya ya mwili na akili kwa vijana na kuimarisha ushiriki wa vijana katika uzalishaji, usindikaji na matumizi ya vyakula vyenye virutubishi muhimu ili kuwa na vijana wenye afya bora.

### 1.2.8. Malezi na Makuzi kwa Vijana

Maadili na tabia njema ni muhimu kwa vijana, jamii na Taifa. Malezi sahihi ya ujana kutoka kwa familia na jamii husaidia kukuza uelewa, uaminifu, kujitegemea, ushirikiano, kujiamini na kuwalinda vijana dhidi ya hofu, mfadhaiko, tabia zisizofaa, na matumizi ya vilevi na dawa za kulevya.

Kwa kutambua umuhimu wa malezi na makuzi kwa vijana, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeandaa na kutekeleza sera, sheria, programu, mikakati na miongozo mbalimbali kwa lengo la kuwa na vijana waadilifu na wawajibikaji kwa familia na Taifa. Miongoni mwa mifumo hiyo ni pamoja na Sheria ya Mtoto, Sura ya 13, Sera ya Maendeleo ya Mtoto (1996) na utoaji wa elimu ya stadi za maisha inayolenga kukuza tabia na mabadiliko ya mawazo kwa vijana na vijana balehe.

Licha ya juhudi zilizochukuliwa, vijana wanaendelea kukabiliwa na changamoto ya mmomonyoko wa maadili. Tabia na vitendo vya baadhi ya vijana vinavyoashiria ukosefu wa maadili ni pamoja na ubakaji, unyanyasaji wa kingono, wizi, na matumizi ya dawa za kulevya. Hali hii inadhihirishwa na kuwepo kwa idadi kubwa ya wafungwa na mahabusu gerezani ambao wana umri wa miaka 15 hadi 35. Kwa mujibu wa Ripoti ya Jeshi la Magereza Tanzania (2022), watu 31,005 walikuwa magerezani mwaka

2021 kati yao vijana wakiwa 22,094 (71.2%). Aidha, kati ya vijana hao, wafungwa ni 12,568 (56.8%) na mahabusu ni 9,526 (43.2%). Halikadhalika, wafungwa vijana 3,827 kati ya 12,568 walikuwa na umri wa miaka 15 hadi 20.

Kwa mujibu wa Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) ilibainika kuwa, migogoro ndani ya ndoa na utengano wa kifamilia ni miongoni mwa vyanzo vya watoto wengi kulelewa na mzazi au mlezi mmoja. Hali hii, imekuwa ikisababisha kukosekana kwa malezi bora kwa watoto na vijana kwa sababu ya kutokuwepo kwa uangalizi wa karibu na kusababisha baadhi yao kujiunga na makundi ya vijana wasio waadilifu ikiwemo watumiaji wa dawa za kulevya.

Vilevile, Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007), ilibaini sababu nyingine zinazochangia mmomonyoko wa maadili kwa vijana ni pamoja na msukumo rika na kufuata mikumbo isiyokuwa na maadili na baadhi ya vijana kukosa stadi za maisha, hali inayopelekea kushindwa kujitambua, kutokuwa na uthubutu na kutofanya maamuzi sahihi. Halikadhalika, matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii na vyombo vya habari; kutokuwepo na mikakati ya kisera ya kulinda na kuimarisha malezi na makuzi; hamu ya kuridhisha wengine na kutaka kutambuliwa na wenzao, na kushuka kwa malezi ya kidini.

Vilevile, ukuaji wa teknolojia, utandawazi na mitandao ya kijamii vimechangia mmomonyoko wa maadili kwa vijana kwa kuiga maisha, mitindo, mila na desturi zisizofaa ikiwemo matumizi ya dawa za kulevya, uhalifu na matatizo mengine ya kisaikolojia. Aidha, njia za asili za kufundisha na kusambaza maadili kwa vijana ikiwemo jando na unyago zimepuuzwa katika baadhi ya jamii, hivyo, kuwanyima fursa vijana ya kupata malezi na makuzi mema ili kuwaepusha kujihusisha na tabia zisizofaa.

Katika kushughulikia changamoto ya mmomonyoko wa maadili kwa vijana, ni muhimu kuwa na mwongozo wa kisera wenye lengo la kuimarisha malezi na makuzi ya vijana na kuweka mazingira wezeshi kwa wadau wa maendeleo ya vijana kutekeleza programu zinazohusiana na malezi na makuzi ya vijana.

### 1.2.9. Taaluma ya Maendeleo ya Vijana

Taaluma ya maendeleo ya vijana inahusisha ujuzi na uwezo wa kuwashirikisha vijana ili kuwawezesha kujiamini, kuwa na mahusiano mema na jamii, kujishughulisha katika masuala ya kiuchumi na uzalishaji mali, kupevuka kiakili na kuwa na maadili mema. Watoa huduma za vijana hufanya kazi Serikalini, taasisi zisizo za Serikali, sekta binafsi, asasi za kiraia na mashirika ya kujitolea ya kitaifa na kimataifa.

Kwa kutambua umuhimu wa taaluma ya maendeleo ya vijana, jitihada mbalimbali zimefanyika ikiwa ni pamoja na kuanzisha kada ya maendeleo ya vijana katika utumishi wa umma, kuweka mfumo wa kisheria kama vile Sheria ya Mashirika Yasiyo

ya Kiserikali Sura ya 56; Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura ya 288, Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287 na Sheria ya Vyama vya Kijamii, Sura ya 337 inayowezesha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Mashirika ya Kidini na Jumuiya za Kijamii kutoa huduma.

Pamoja na jitihada zilizofanyika, taaluma ya maendeleo ya vijana inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa mfumo wa kisheria unaoweka viwango vya maadili na vigezo vya umahiri vya kuzingatiwa na watoa huduma za maendeleo ya vijana. Pia, taasisi nyingi za vijana nchini zina madawati yanayohudumia vijana, lakini, maafisa wengi katika madawati hayo hawana taaluma ya maendeleo ya vijana na sifa za kada hiyo, hali inayosababisha utoaji wa huduma za maendeleo ya vijana pasipo kuzingatia misingi ya taaluma.

Kwa upande mwingine, Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) ilibaini kuwa, pamoja na umuhimu wa taaluma ya maendeleo ya vijana nchini, suala hilo halikuzingatiwa katika sera na kusababisha kukosekana kwa mwongozo mahsusi wa kisera wa kukuza na kuimarisha taaluma hii. Hali hii imesababisha upungufu mkubwa wa maafisa maendeleo ya vijana ambapo ni nafasi 17 tu zimejazwa kati ya 26 zinazohitajika katika ngazi ya Mkoa sawa na 65%. Aidha, katika ngazi ya Halmashauri, nafasi 35 kati ya 184 sawa na 19% zimejazwa hali inayoathiri utoaji wa huduma za maendeleo ya vijana katika utumishi wa umma.

Kwa kuzingatia changamoto zilizoainishwa kuhusiana na taaluma ya maendeleo ya vijana, ni muhimu kuwa na mwongozo mahsusi wa kisera utakaowezesha kutambuliwa na kuendelezwa kwa taaluma ya maendeleo ya vijana.

### 1.2.10. Uongozi na Utawala

Uongozi na utawala ni miongoni mwa misingi na nyenzo muhimu katika maendeleo na uwezeshaji wa vijana. Katika kuhakikisha kwamba masuala yanayowahusu vijana na makundi mengine yanapatiwa ufumbuzi ipasavyo, ni muhimu vijana wenyewe washiriki kikamilifu katika michakato ya maamuzi na kupewa fursa za uongozi badala ya kuwa watazamaji.

Hivyo basi, mifumo mbalimbali ya kisera, kisheria, kimkakati na miongozo yenye lengo la kukuza uongozi na utawala kwa vijana imeendelea kutekelezwa na serikali kwa kushirikiana na wadau. Miongoni mwa mifumo hiyo ni Sera ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2009 na Sheria Sura ya 103; Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Na.16, 2004; Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura ya 410; Sheria ya Asasi Zisizo za Kiserikali Sura ya 56; Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura ya 288, Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287 na Sheria ya Vyama vya Kijamii, Sura ya 337. Hata hivyo, mifumo yote hii inawachukulia vijana kama sehemu ndogo ya watu badala ya walengwa wakuu wanaohitaji uangalizi maalum, usaidizi na huduma.

Pamoja na jitihada zilizochukuliwa na serikali, ushiriki wa vijana katika masuala ya uongozi na utawala hususani katika ngazi za maamuzi ni wa kiwango cha chini. Hali hii inaweza kuwa inasababishwa na kukosekana kwa mwongozo wa kisera wa kuwaandaa vijana kushika nafasi za uongozi na kushiriki kwenye vyombo mbalimbali vya maamuzi. Aidha, programu za kuhamasisha uongozi kwa vijana ni chache. Vilevile, hata zilizopo si rahisi kufikiwa na vijana na uendelevu wake bado ni kikwazo kikubwa katika ukuaji wake katika kufikia malengo tarajiwa.  Ingawa serikali imeweka mifumo mbalimbali yenye taarifa na takwimu zinazohusu shughuli mbalimbali ikiwemo masuala ya vijana, bado mifumo hiyo siyo unganifu na usahihi wa baadhi ya taarifa na takwimu hauridhishi kutokana na changamoto katika ukusanyaji, uhakiki, uchambuzi na uhifadhi wake.

Katika kutatua changamoto zinazohusiana na uongozi na utawala kwa vijana, kuna umuhimu wa kuwa na mwongozo wa kisera unaohakikisha masuala ya uongozi na utawala yanajumuishwa katika mipango mbalimbali ya maendeleo ya vijana na kuhakikisha wanashirikishwa kikamilifu katika ngazi zote za maamuzi.

**1.2.11. Masuala ya Vijana na Jinsia**

Usawa wa kijinsia ni miongoni mwa vipengele muhimu katika maendeleo na uwezeshaji wa vijana. Suala la usawa wa kijinsia kwa vijana huleta uwiano ulio sawa wa ushiriki wa vijana wa kike na kiume katika mipango mbalimbali kwa lengo la kunufaika na fursa zilizopo bila upendeleo.

Kwa kutambua umuhimu wa usawa wa kijinsia kwa vijana, Serikali imeandaa na kutekeleza sera, sheria, mikakati na miongozo mbalimbali inayoshughulikia masuala ya jinsia kwa vijana ikiwa ni pamoja na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000); kuridhia na kutekeleza Mkataba wa Kutokomeza Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake; na Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto 2017/18-2021/22.

Juhudi nyingine ni uanzishwaji wa madawati ya uratibu wa masuala ya jinsia katika Wizara, Idara na Wakala, na uanzishwaji wa Dawati la Jinsia na Watoto katika vituo vya polisi nchini, na utoaji wa mafunzo ya kukabiliana na unyanyasaji kwa watoto na ukatili wa kijinsia. Kupitia utekelezaji wa mipango hiyo, uwiano wa wanawake katika nafasi za uongozi wa juu na wa kati umeongezeka kutoka 23.3% mwaka 2014 hadi 28.0% mwaka 2021. Aidha, umepunguza pengo la kijinsia katika majukumu ya kufanya maamuzi mahali pa kazi na kupungua kwa kiwango cha wasiojua kusoma na kuandika miongoni mwa wanawake kutoka 25.1% mwaka 2014 hadi 21.3% mwaka 2021 (ILFS, 2021).

Licha ya jitihada na mafanikio yaliyopatikana, bado changamoto ya usawa kijinsia kwa vijana imeendelea kuwepo katika maeneo mbalimbali. Kwa mfano, katika eneo la ajira, utafiti wa Nguvu Kazi, 2021 ulibaini kuwa, kiwango cha ukosefu wa ajira kwa

wanawake kiliongezeka kutoka 12.6% mwaka 2006 hadi 12.7% mwaka 2021 wakati kwa wanaume kilipungua kutoka 10.7% mwaka 2006 hadi 5.8% mwaka 2021.

Aidha, uwiano wa wasio katika ajira wala elimu au mafunzo kwa vijana wa kike ni 22.9% ikilinganishwa na 10.8% kwa vijana wa kiume. Takwimu hizi zinaashiria vijana wa kike wanakabiliwa zaidi na changamoto ya upatikanaji wa ajira ikilinganishwa na vijana wa kiume. Kwa upande wa elimu, utafiti wa Hali ya Kipato cha Kaya (HBS) 2017/18 unaonesha kuwa 22.5% ya wanawake walikuwa na uwezekano mkubwa wa kukosa elimu rasmi ikilinganishwa na 12.7% kwa wanaume.

Vilevile, Taarifa ya SIGI ya mwaka 2022 ilibaini kuwa 8.1% ya vijana wa kike walifanyiwa ukatili wa kimwili, 16.3% ukatili wa kijinsia na 8.2% ukatili wakati wa ujauzito. Aidha, msichana mmoja kati ya watatu aliolewa akiwa na umri wa miaka 18 na mimba za utotoni ni 22% kwa wale wenye umri wa miaka 15 - 19. Ukosefu wa ulinzi na unyanyasaji wa kijinsia umekuwa na athari mbaya kwa vijana, hasa vijana wa kike, ambao wanajumuisha idadi kubwa ya waathiriwa wote.

Kadhalika, Taarifa ya SIGI, Tanzania ya mwaka 2022 ilibaini kuwa, ndoa za utotoni ni tatizo kubwa miongoni mwa vijana wa kike, ambapo hali hiyo ipo juu katika baadhi ya mikoa na maeneo ya vijijini. Mathalani, mwaka 2021, 16% ya vijana wa kike wenye umri kati ya miaka 20 hadi 24 walikuwa wameolewa, kuachwa au kufiwa kabla ya umri wa miaka 18 ikilinganishwa na 2% ya vijana wa kiume wenye umri huo waliokuwa kwenye ndoa, kufiwa au kuachika kabla ya umri wa miaka 18. Ndoa katika umri mdogo kwa vijana wa kike zinasababishwa na baadhi ya jamii kuona ni sahihi kwa mwanamke kuolewa kabla ya umri wa miaka 18 na uwepo wa mitazamo tofauti kuhusu umri unaofaa kwa vijana wa kike na kiume kuingia kwenye ndoa (Taarifa ya SIGI, Tanzania, 2022).

Katika kuhakikisha uwepo wa usawa wa kijinsia kwa vijana, upo umuhimu wa kuwa na mwongozo mahsusi wa kisera ambao utahakikisha ujumuishaji wa masuala ya jinsia katika afua zote za maendeleo ya vijana nchini ili kukabiliana na mila zote za kibaguzi hususani zinazohusu kukosekana kwa usawa wa kijinsia.

### 1.2.12. Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira
Vijana ni miongoni mwa rasilimali muhimu katika usimamizi na utunzaji wa mazingira nchini. Vilevile, vijana ni kundi lenye wajibu wa kuhakikisha mazingira yanatunzwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Kwa kuzingatia umuhimu wa hifadhi ya mazingira, Serikali imeweka mifumo mbalimbali ikiwemo sera, sheria, kanuni, mikakati na miongozo inayohimiza usimamizi na utunzaji wa mazingira. Miongoni mwa mifumo hiyo ni pamoja na Sera ya Taifa ya Mazingira (2021); Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191; Mpango wa Kitaifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (2014

– 2018); Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 -2032); Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (2022 – 2026); Mkakati wa Kudhibiti Viumbe Vamizi (2019 -2029); Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Taka Hatarishi (2019) na Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa ya Ukaa Kutokana na Ukataji na Uharibifu wa Misitu (MKUHUMI) na Mpango Kazi wake. Aidha, kufuatia umuhimu huu, Serikali imeungana na mataifa mengine kuadhimisha siku ya Mazingira Duniani na Kampeni mbalimbali zinazolenga kuhifadhi mazingira.

Kutokana na utekelezaji wa sera, sheria, kanuni, mikakati na miongozo, matumizi ya kuni kama nishati kuu ya kupikia yamepungua kutoka 73.1% kwa kaya mwaka 2007 hadi 60.9% mwaka 2018 (HBS, 2017/18). Pia, Serikali imeanzisha Mfuko wa Kuendeleza Misitu Tanzania chini ya Sheria ya Misitu Sura ya 323 kwa lengo la kukuza usimamizi wa mazingira ambapo jumla ya miradi 514 ikiwemo ya vijana imenufaika na miti zaidi ya milioni mbili imepandwa. Mafanikio mengine ni kuongezeka kwa matumizi ya nishati mbadala ikijumuisha umeme, gesi na gesi asilia. Kwa mujibu wa HBS, 2017-18 matumizi ya gesi ya viwandani yalikuwa 3.2%, umeme 2.1%, mafuta ya taa 1.3% na nishati ya jua 1.1%. Vilevile, matumizi ya kuni kwa kupikia yalipungua kutoka 73.1% mwaka 2007 hadi 60.9% mwaka (HBS, 2017/18).

Pamoja na mafanikio hayo, vijana wameendelea kufanya shughuli zinazochangia uharibifu wa mazingira katika jitihada za kujitafutia kipato. Miongoni mwa shughuli hizo ni pamoja na uchomaji mkaa, utengenezaji matofali na ukataji wa miti holela kwa ajili ya mbao na kuni. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 takriban 56% ya kaya zinatumia kuni na 25.9% zinatumia mkaa kama chanzo kikuu cha nishati ya kupikia. Vilevile Takwimu zinaonesha kuwa kasi ya uvunaji misitu nchini kwa miaka 10 iliyopita ni kati ya hekta 300,000 hadi 400,000 kwa mwaka.

Kuendelea kutumia kuni na mkaa kama vyanzo vikuu vya nishati ya kupikia kunasababisha uharibifu wa mazingira kwa kukata miti, kuharibu udongo na kutoa gesi ukaa ambavyo vina athari kwenye bioanuai, mabadiliko ya tabia nchi na uendelevu wa maliasili. Aidha, kuna hali ya kukosekana kwa uwiano kati ya kasi ya ukataji na upandaji miti nchini, na kwa kiasi kikubwa imechangia kutokea kwa athari kubwa za mabadiliko ya tabianchi.

Kwa kuzingatia umuhimu na mchango wa vijana katika usimamizi na utunzaji wa mazingira, kuna haja ya kuwa na mwongozo mahsusi wa kisera ambao utakuza na kuimarisha ushiriki wa vijana katika usimamizi na utunzaji wa mazingira nchini.

**1.2.13. Vijana Wenye Ulemavu**

Vijana wenye ulemavu ni kundi muhimu kwa maendeleo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kundi hili hujumuisha vijana wenye changamoto za kimwili, kiakili, na kihisia za muda mrefu ambazo zinapoingiliana na vikwazo vya kimitazamo, kimazingira na kitaasisi huwa ni vigumu kwao kushiriki kikamilifu na kwa ufanisi

katika shughuli za kawaida za kijamii. Pia, ni kundi lenye mahitaji na changamoto maalumu ikilinganishwa na vijana wasiokuwa na ulemavu. Hivyo, ni muhimu kutoa fursa kwa vijana wenye ulemavu kwa kuhakikisha ushiriki thabiti katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Serikali imeweka sera, sheria, mikakati na miongozo mbalimbali yenye lengo la kukuza na kuimarisha utoaji wa huduma kwa vijana wenye ulemavu zikiwemo kuandaa na kutekeleza Mwongozo wa Kitaifa wa Utambuzi wa Mapema na Afua Stahiki kwa Watoto wenye Ulemavu (2021); Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Sura ya 183; Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura ya 410; Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290; Sera ya Huduma na Mandeleo kwa Watu Wenye Ulemavu (2004); Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu (2006), na Mkataba wa Marrakesh (2013).

Kutokana na utekelezaji wa juhudi hizo, kiwango cha ajira kwa watu wenye ulemavu kimeongezeka kutoka 59.1% mwaka 2014 hadi 63.2% mwaka 2021 na ukosefu wa ajira umepungua kutoka 12.4% mwaka 2014 hadi 6.0% mwaka 2021 (ILFS, 2021). Vilevile, kuboreshwa kwa miundombinu katika majengo ya umma na ya binafsi na maeneo mengine ya utoaji huduma kwa umma (Tathmini ya Sera, 2007) na utengaji wa 10% kati ya 30% ya ununuzi wa umma kwa watu wenye ulemavu (NEEC, 2005 - 2015)

Mafanikio mengine ni pamoja na utoaji wa ujuzi na mafunzo ya ufundi kwa vijana wenye ulemavu kupitia programu ya kukuza ujuzi na vyuo vya ufundi stadi na marekebisho ambapo kwa wastani wa wanafunzi 1,000 hudahiliwa kwa mwaka (FYDP III) na vikundi zaidi ya 1,906 vya watu wenye ulemavu wakiwemo vijana vimepatiwa mikopo ya masharti nafuu (NEEC, 2023). Aidha, Tathmini ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) inaonesha kuwa uteuzi au ushirikishwaji wa vijana wenye ulemavu katika vyombo vya maamuzi umeongezeka na ushiriki wa vijana wenye ulemavu katika masuala ya uchaguzi kutokana na uwepo wa mazingira rafiki kama vile karatasi za kupigia kura zenye maandishi ya breli na yaliyokuzwa (NEC, Ripoti ya Uchaguzi, 2020).

Serikali imefanya juhudi na kupata mafanikio ingawa bado idadi ya vijana wenye ulemavu waliofikiwa na programu za uwezeshaji kiuchumi ni ndogo ikilinganishwa na vijana wasiokuwa na ulemavu na kuwepo kwa mazingira yasiyokuwa rafiki katika baadhi ya maeneo ya mijini na vijijini. Hali hii imepelekea ushiriki hafifu kwa vijana wenye ulemavu katika shughuli za kila siku za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Aidha, watu wenye ulemavu, hasa wanawake na vijana, wanawakilishwa katika vyombo vya maamuzi ndani na nje ya nchi kwa kiwango kidogo. Hali hii kwa kiasi kikubwa inapunguza uwezo wao wa kushiriki na kushawishi maamuzi yanayoathiri maisha yao.

Ili kukabiliana na changamoto hizo, kuna umuhimu wa kuwa na mwongozo mahsusi wa kisera kwa lengo la kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa vijana wenye ulemavu katika masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi na kuimarisha ujumuishaji wa masuala ya vijana wenye ulemavu katika sera za kisekta, mikakati, mipango, programu na miradi ya serikali na wadau wengine.

## 2.1. Umuhimu wa Sera

Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) iliandaliwa kwa lengo la kuwawezesha na kuwaongoza vijana na wadau wengine kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Utekelezaji wa sera hiyo umefanyika kwa kuzingatia sera za kisekta, sheria, kanuni, taratibu, miongozo na mipango. Ingawa kumekuwa na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa sera hiyo, Taarifa ya Tathmini ya Utekelezaji wa Sera hii (2022) ilibaini upungufu katika utekelezaji wake. Upungufu huo ni pamoja na kutofafanuliwa kwa baadhi ya maeneo ya msingi kama vile TEHAMA; elimu na mafunzo; huduma za afya; ushiriki wa vijana na utawala bora; dhima iliyopo kutoa mwelekeo usioendana na dira ya sera; kukosekana kwa mkakati wa utekelezaji na baadhi ya matamko ya kisera kutojibu changamoto zilizoainishwa kwenye baadhi ya masuala kama vile fasili ya kijana, ushirikiano wa kikanda na utandawazi na haki za vijana.

Mapungufu mengine ni pamoja na wadau kukosa mwelekeo wa pamoja katika kushughulikia changamoto zinazowakabili vijana; kuwekwa kwa jitihada zisizotatua changamoto zilizokusudiwa kama vile ukosefu wa ajira; vijana kuwa na kiwango kidogo cha ujuzi wa juu na wa kati; ongezeko la vijana walioajiriwa katika sekta isiyo rasmi wanaofanya kazi katika mazingira hatarishi; baadhi ya vijana kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya; kukosekana kwa mfumo madhubuti wa kuwatambua na kuwaandaa vijana kuwa viongozi; na mfumo usiokidhi wa uratibu na usimamizi wa shughuli za maendeleo ya vijana na uwezekano wa kutumia rasilimali katika shughuli zisizochangia ipasavyo ufikiaji wa malengo ya sera. Aidha vijana wameendelea kuwa mawakala wa uharibifu wa mazingira katika jitihada za kujitafutia kipato; mmomonyoko wa maadili na uwepo wa mimba katika umri mdogo.

Kwa upande mwingine, kumekuwepo na Mikataba, Makubaliano na Itifaki za Kikanda na Kimataifa ambazo zilipitishwa na kuanza kutumika baada ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) zinazoainisha ushiriki wa vijana kwenye masuala ya amani na usalama; lishe; utambuzi na uendelezaji wa vijana wavumbuzi na wabunifu; utambuzi wa taaluma ya maendeleo ya vijana na uanzishwaji wa programu za mafunzo.

Kwa kuzingatia upungufu wa sera na changamoto zilizobainishwa, Serikali imefanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007) na kuandaa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007), Toleo la Mwaka 2024 ili kukidhi mahitaji ya sasa na kutoa mwelekeo wa masuala ya vijana kwa manufaa ya taifa.

## 2.2. Dira

Kuwa na vijana wenye ujuzi, ubunifu, ufahamu na matumizi sahihi ya teknolojia, waliowezeshwa, waliolelewa vyema, wazalendo na wawajibikaji.

### 2.3. Dhima
Kuweka mfumo fanisi wa kitaasisi na kisheria ulioratibiwa vyema kwa maendeleo endelevu ya vijana kupitia uwezeshaji wa kijamii, kisiasa na kiuchumi; ujuzi husika; matumizi bora ya rasilimali za taifa na kukuza ushiriki katika fursa za kitaifa, kikanda na kimataifa.

### 2.4. Malengo ya Sera

#### 2.4.1. Lengo Kuu
Kutoa mwongozo kwa wadau wa maendeleo ya vijana katika uwezeshaji na ushiriki wa vijana kwenye shughuli za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

#### 2.4.2. Malengo Mahsusi
Malengo mahsusi ya sera ni:

(a) Kukuza elimu na ujuzi unaoendana na mahitaji ya soko la ajira;
(b) Kukuza uvumbuzi na ubunifu kwa vijana ili kuibua na kuendeleza vipaji vyao;
(c) Kuimarisha ujuzi wa kidijitali, ufikivu na upatikanaji wa bidhaa na huduma za kidijitali zinazohitajika kwa vijana kwa gharama nafuu;
(d) Kukuza fursa za kujiajiri au kuajiriwa kwa vijana;
(e) Kukuza ushiriki wa vijana katika sekta za kijamii na kiuchumi;
(f) Kukuza uzalendo, utaifa na kujitolea kwa vijana;
(g) Kuwa na kijana mwenye afya bora;
(h) Kukuza tamaduni na maadili mema kwa malezi na makuzi bora ya vijana;
(i) Kukuza taaluma ya maendeleo ya vijana;
(j) Kuimarisha ushiriki wa vijana katika uongozi na vyombo vya maamuzi;
(k) Kuhakikisha uwepo wa uwiano wa kijinsia kwa vijana;
(l) Kuhakikisha ushiriki wenye tija kwa vijana katika usimamizi na uhifadhi wa mazingira; na
(m) Kuimarisha ujumuishwaji wa masuala ya vijana wenye ulemavu katika mipango na programu za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

## 3.1. Elimu na Ujuzi kwa Vijana

**Maelezo**
Elimu bora inajumuisha maarifa na ujuzi unaoendana na mahitaji ya shughuli za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Elimu na ujuzi husika kwa vijana huongeza tija katika uzalishaji na utoaji wa huduma mbalimbali kwa jamii. Pamoja na umuhimu wa elimu na ujuzi, vijana wengi bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kuwa na ujuzi usioendana na mahitaji ya soko la ajira; kutopenda kujisomea na kutafuta maarifa mapya; idadi ndogo ya vijana waliofikiwa na programu za kukuza ujuzi na uwepo wa fursa za mafunzo ya ufundi stadi zisizotosheleza mahitaji.

**Lengo**
Kukuza elimu na ujuzi unaoendana na mahitaji ya soko la ajira kwa vijana.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:

1.1.1. Kuboresha mfumo wa upatikanaji wa elimu na ujuzi unaoendana na mahitaji ya soko la ajira kwa gharama nafuu hususan kwa vijana waliopo maeneo ya vijijini;
1.1.2. Kuimarisha elimu ya kujitegemea na programu za mafunzo ya ujuzi kwa vijana;
1.1.3. Kutoa na kuimarisha ujuzi tepe, stadi za maisha na mafunzo endelevu kwa vijana; na
1.1.4. Kuimarisha na kuendeleza mafunzo ya ujasiriamali kwa vitendo kwa vijana.

## 3.2. Uvumbuzi na Ubunifu kwa Vijana

**Maelezo**
Uvumbuzi na ubunifu ni miongoni mwa vichocheo muhimu vya maendeleo ya vijana na uchumi kwa maendeleo endelevu ya nchi. Hata hivyo, kumekuwapo na changamoto zinazoathiri ushiriki na ushirikishwaji wa vijana katika uvumbuzi na ubunifu zikiwemo uhaba wa miundombinu na fursa za uendelezaji wa masuala ya uvumbuzi na ubunifu kwa vijana; ushiriki mdogo wa vijana katika mfumo wa uvumbuzi na ubunifu na ukosefu wa ujuzi wa kutosha; kuwa na rasilimali zisizotosheleza mitaji kwa wavumbuzi na wabunifu; vijana kuwa mbali na taasisi za utafiti na maendeleo na matumizi madogo ya sayansi na teknolojia katika mfumo wa ubunifu wa msingi.

**Lengo**
Kukuza uvumbuzi na ubunifu kwa vijana ili kuibua na kuendeleza vipaji.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:

1.1.1. Kukuza na kuendeleza uvumbuzi, vipaji na ubunifu kwa vijana;
1.1.2. Kukuza ushiriki wa sekta binafsi katika kuendeleza uvumbuzi na ubunifu wa vijana;
1.1.3. Kuhakikisha matumizi bora na sahihi ya sayansi na teknolojia katika kukuza uvumbuzi na ubunifu wa vijana;
1.1.4. kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kutambua na kuendeleza uvumbuzi na ubunifu wa vijana; na
1.1.5. Kukuza hakimiliki ikiwemo hakimiliki dhihini na hataza za wavumbuzi na wabunifu vijana.

## 3.3. Vijana na Mapinduzi ya Kidijitali

**Maelezo**
Mapinduzi ya kidijitali kwa kiwango kikubwa yamebadilisha maisha ya vijana kutokana na matumizi ya intaneti na mifumo ya upatikanaji wa huduma hizo kama vile kompyuta mpakato, vishikwambi na simu janja, pamoja na majukwaa ya mitandao ya kijamii na programu za kutuma ujumbe ambazo zimekuwa muhimu kwa maisha ya vijana. Hata hivyo, vijana wengi hawajaandaliwa vyema katika kutumia fursa zinazotokana na mapinduzi ya kidijitali. Hali hii inasababisha matumizi yasiyo ya kimaadili ya teknolojia ya habari na mawasiliano na mitandao ya kijamii na ushiriki hafifu wa vijana katika uchumi wa kidijitali hasa vijijini.

**Lengo**
Kuimarisha ujuzi wa kidijitali, ufikivu na upatikanaji wa bidhaa na huduma za kidijitali zinazohitajika kwa vijana kwa gharama nafuu.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:

1.1.1. Kuhakikisha upatikanaji na ufikivu wa huduma za intaneti zenye uhakika na kwa bei nafuu kwa vijana hususan maeneo ya vijijini;
1.1.2. Kuimarisha programu za mafunzo ya kidijitali katika ngazi zote za elimu;
1.1.3. Kukuza uelewa wa vijana kuhusu mapinduzi ya kidijitali ili waweze kushiriki na kunufaika na fursa zitokanazo na mabadiliko ya teknolojia; na
1.1.4. Kuhakikisha vijana wana ujuzi stahiki na taarifa sahihi kuhusu matumizi yenye maadili ya teknolojia ya habari, mawasiliano na mitandao ya kijamii.

## 3.4. Ajira kwa Vijana

**Maelezo**
Ajira ni nyenzo muhimu kwa maendeleo ya mtu binafsi, jamii na taifa kwa ujumla. Pamoja na umuhimu wa ajira, vijana wengi wameendelea kukabiliwa na changamoto ya ukosefu wa ajira ambayo ni kubwa kwa vijana wa kike kuliko wa kiume na ni kubwa katika maeneo ya mijini ikilinganishwa na vijijini.

**Lengo**
Kukuza fursa za kujiajiri au kuajiriwa kwa vijana.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:

1.1.1. Kukuza uchumi ili uweze kuzalisha fursa za kutosha na endelevu za ajira kwa vijana;
1.1.2. Kuweka mifumo itakayowezesha vijana kupata uzoefu wa vitendo kupitia programu za mafunzo na stadi za kazi;
1.1.3. Kukuza utamaduni wa ujasiriamali, mafunzo ya ufundi stadi, uelewa wa masuala ya kifedha na mazingira wezeshi ya biashara ili vijana waweze kujiajiri na kuajiriwa;
1.1.4. Kukuza ujuzi na umahiri utakaowawezesha vijana kunufaika na fursa za ajira zinazotokana na ukuaji wa sekta za kimkakati katika uchumi; na
1.1.5. Kuweka mfumo utakaowawezesha wadau wa sekta zote kushiriki kikamilifu kukuza fursa za ajira.

### 3.5. Ushiriki wa Vijana Katika Sekta za Kijamii na Kiuchumi

**Maelezo**

Ushiriki wa vijana katika sekta za kijamii na kiuchumi unahusisha uwezo wa vijana kumiliki, kuongoza, kusimamia na kuendesha shughuli mbalimbali za maendeleo. Pamoja na umuhimu huo, vijana wameendelea kukabiliwa na mifumo duni na fursa chache za upatikanaji wa mitaji, masoko na huduma za ushauri; idadi kubwa ya vijana kujihusisha na shughuli za kiuchumi na kumiliki rasilimali nje ya mfumo rasmi na kukosekana kwa mfumo wenye ufanisi wa kutambua mchango wa vijana wanaoishi nje ya nchi.

**Lengo**

Kukuza ushiriki wa vijana katika sekta za kijamii na kiuchumi.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:

1.1.1. Kuhakikisha uwepo wa mifumo wezeshi na fursa za upatikanaji wa mitaji, masoko, huduma za kinga ya jamii na ushauri kwa vijana;
1.1.2. Kuimarisha umiliki, usimamizi, na uwezo wa vijana katika kuweka akiba, uwekezaji, uzalishaji na uendeshaji wa biashara kwenye sekta za kijamii na kiuchumi ndani na nje ya nchi;
1.1.3. Kuweka mazingira wezeshi kwa vijana kuanzisha na kuendesha ujasiriamali na biashara binafsi au kwa ubia;
1.1.4. Kuhakikisha uwepo wa mfumo wa kutambua na kuwezesha ushiriki wa vijana wanaoishi nje ya nchi (diaspora) kwenye masuala ya maendeleo ya vijana;
1.1.5. Kuimarisha urasimishaji wa sekta isiyo rasmi; na
1.1.6. Kukuza ushiriki wa vijana katika sekta muhimu za kijamii na kiuchumi ikiwemo kilimo; utamaduni sanaa na michezo na sekta zingine muhimu.

### 3.6. Uzalendo, Kujitolea na Utaifa

**Maelezo**

Vijana wenye uzalendo, kujitolea na utaifa ni hazina kubwa katika kukuza umoja, mshikamano, amani, usalama na utulivu wa kisiasa na kiuchumi nchini. Hata hivyo, hali ya uzalendo na utaifa kwa vijana wengi imeendelea kushuka kutokana na mifumo iliyokuwa inatumika kujenga sifa hizi kutofanya kazi ipasavyo.

Hali hii imesababisha uwepo wa vijana wengi wasio wazalendo, kuzorota kwa maadili, kuongezeka kwa uhalifu, uharibifu wa mali, uvunjifu wa amani na ukosefu wa usalama wa mali na raia. Kadhalika, vijana wanakabiliwa na tabia ya kukosa moyo wa kujitolea katika shughuli za ujenzi wa Taifa, kutoshiriki ipasavyo katika kutoa huduma za jamii na shughuli za uokoaji wakati wa maafa ya kitaifa, ajali na dharura. Aidha, kukosekana kwa mkakati wa kitaifa wa kujitolea, kumeleta changamoto katika kuratibu na kukuza moyo wa kujitolea.

**Lengo**
Kukuza uzalendo, moyo wa kujitolea na utaifa kwa vijana

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:

1.1.1. Kuanzisha na kuimarisha mifumo ya kupandikiza uzalendo, utaifa na moyo wa kujitolea kwa vijana;
1.1.2. Kukuza uzalendo, utaifa, na moyo kujitolea kwa vijana katika hatua mbalimbali za elimu, malezi na makuzi;
1.1.3. Kuhakikisha programu za uongozi kwa vijana zinafungamanisha masuala yanayohusu uzalendo na utaifa; na
1.1.4. Kukuza ushiriki wa vijana katika masuala yanayohusu amani na usalama ili kuimarisha utulivu wa kisiasa, kijamii na kiuchumi.

### 3.7. Afya na Lishe

**Maelezo**
Afya na lishe ni masuala ya msingi na mtambuka ambayo yana mchango mkubwa katika ustawi wa vijana na kuwawezesha kushiriki katika shughuli za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Pamoja na umuhimu huo, vijana wengi wanakabiliwa na changamoto mbalimbali za kiafya ikiwemo mimba za utotoni, afya ya uzazi, VVU na UKIMWI na matumizi ya dawa za kulevya.  Changamoto nyingine ni kuibuka kwa magonjwa yasiyoambukiza; lishe duni; na afya ya akili, hali inayosababisha udumavu kwa vijana na kuathiri mfumo wa afya ya uzazi na kupelekea kushindwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji.

**Lengo**
Kuwa na kijana mwenye afya bora.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:

1.1.1. Kuhakikisha uwepo wa mifumo toshelevu inayowezesha vijana kupata elimu ya stadi za maisha, afya ya uzazi na huduma nyingine saidizi.
1.1.2. Kuimarisha mifumo ya udhibiti wa dawa za kulevya, VVU na UKIMWI na mimba katika umri mdogo;
1.1.3. Kuimarisha programu za kukabiliana na magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza na afya ya akili kwa vijana;
1.1.4. Kuongeza uelewa na uhamasishaji wa vijana juu ya magonjwa yanayohusiana na mtindo wa maisha; na
1.1.5. Kukuza programu za lishe, ikiwa ni pamoja na elimu, ulaji bora na urutubishaji wa vyakula

### 3.8. Malezi na Makuzi kwa Vijana

**Maelezo**

Maadili na tabia njema ni muhimu kwa vijana, jamii na taifa. Malezi sahihi ya ujana kutoka kwa familia na jamii husaidia kukuza uelewa, uaminifu, kujitegemea, ushirikiano na kujiamini. Pamoja na umuhimu wa maadili na tabia njema, baadhi ya vijana wamekuwa na tabia na vitendo vinavyoashiria ukosefu wa maadili kama vile ubakaji, unyanyasaji wa kingono, wizi, na matumizi ya dawa za kulevya. Vilevile, vijana wanakabiliwa na changamoto ya kushiriki kwenye vitendo vinavyoshusha utu wao na kupuuzwa kwa njia za asili za kufundisha na kusambaza maadili mema kwa vijana ikiwemo jando na unyago ambavyo vimechangia kuwepo kwa mmomonyoko wa maadili kwa vijana kwa sababu ya kuiga maisha, mitindo, mila na desturi zisizofaa.

**Lengo**

Kukuza tamaduni bora na maadili mema kwa malezi na makuzi bora ya vijana.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:

1.1.1. Kuimarisha familia na jamii kama misingi muhimu ya malezi na makuzi kwa vijana;
1.1.2. Kukuza mabadiliko chanya ya tabia kwa vijana;
1.1.3. Kukuza desturi za kitamaduni zinazochangia maadili na mienendo bora kwa vijana; na
1.1.4. Kuimarisha mifumo inayotumika kufundisha na kusambaza maadili mema kwa vijana.

### 3.9. Taaluma ya Maendeleo ya Vijana

**Maelezo**
Taaluma ya maendeleo ya vijana inahusisha ujuzi na uwezo wa kuwashirikisha vijana ili kuwawezesha kujiamini, kuwa na mahusiano mema na jamii, kujishughulisha katika masuala ya kiuchumi na uzalishaji mali, kupevuka kiakili na kuwa na maadili mema. Pamoja na umuhimu wa taaluma ya maendeleo ya vijana, hakuna mfumo wa kisheria au kikanuni unaoweka viwango vya maadili na vigezo vya umahiri vya kuzingatiwa kwa watoa huduma za maendeleo ya vijana mahiri.

**Lengo**
Kukuza taaluma ya maendeleo ya vijana.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:

1.1.1. Kuhakikisha uwepo wa mfumo wa utambuzi wa taaluma ya maendeleo ya vijana ili kuwa na rasilimaliwatu yenye umahiri katika utoaji wa huduma kwa vijana nchini;
1.1.2. Kuweka mfumo wa kisheria na kikanuni unaoweka viwango vya maadili na vigezo vya kuzingatiwa na watoa huduma za maendeleo ya vijana nchini; na
1.1.3. Kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa huduma za maendeleo ya vijana.

### 3.10. Uongozi na Utawala

**Maelezo**
Uongozi na utawala ni miongoni mwa misingi na nyenzo muhimu katika maendeleo na uwezeshaji wa vijana. Pamoja na umuhimu huo, ushiriki wa vijana katika masuala ya uongozi na utawala hususani katika ngazi za maamuzi ndani na nje ya nchi si wa kuridhisha. Hali hii inatokana na uwepo wa mifumo dhaifu katika kuwaandaa vijana kushika nafasi za uongozi na kushiriki kwenye vyombo mbalimbali vya maamuzi.

**Lengo**
Kuimarisha ushiriki wa vijana katika uongozi na utawala kwenye vyombo vya maamuzi.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:

1.1.1. Kupandikiza tunu za taifa na kanuni za utawala bora kwa vijana;
1.1.2. Kukuza ushiriki wa vijana katika siasa, uongozi na vyombo vya maamuzi kitaifa na kimataifa;
1.1.3. Kuhakikisha uwepo wa mfumo unganifu wa taarifa na takwimu zinazohusu maendeleo ya vijana katika ngazi zote;
1.1.4. Kuimarisha utafiti na utekelezaji wa matokeo ya tafiti katika utoaji wa huduma mbalimbali za maendeleo na ustawi wa vijana nchini;
1.1.5. Kuweka mazingira yatakayowezesha mtandao wa mashirika ya vijana na asasi za kiraia kushiriki katika kubuni, kutekeleza na kufuatilia mipango ya maendeleo ya vijana; na
1.1.6. Kuimarisha mfumo wa uratibu wa shughuli za maendeleo ya vijana zinazotekelezwa katika sekta na taasisi mbalimbali nchini.

### 3.11. Masuala ya Vijana na Jinsia

**Maelezo**
Usawa wa kijinsia ni miongoni mwa vipengele muhimu katika maendeleo na uwezeshaji wa vijana. Pamoja na umuhimu wa usawa kwa vijana, bado changamoto ya usawa wa kijinsia kwa vijana imeendelea kuwepo katika maeneo mbalimbali. vijana wa kike wanakabiliwa zaidi na changamoto ya kufanyiwa ukatili wa kijinsia na hatari ya ndoa za utotoni kuliko wa kiume. Vilevile, wanakabiliwa na changamoto katika kumiliki ardhi na ufikivu wa mifumo ya kifedha, hali inayochangia kuendelea kuwepo kwa changamoto ya usawa wa kijinsia.

**Lengo**
Kuhakikisha uwepo wa uwiano mzuri wa kijinsia kwa vijana.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:

1.1.1. Kukuza usawa wa umiliki wa rasilimali kwa vijana wa kiume na kike.
1.1.2. Kuimarisha usawa katika ushiriki wa vijana wa kiume na wa kike kwenye shughuli za kijamii, kisiasa na kiuchumi; na
1.1.3. Kuimarisha mifumo ya udhibiti wa aina zote za ubaguzi na unyanyasaji wa kijinsia kwa vijana.

### 3.12.Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira

**Maelezo**
Vijana ni miongoni mwa rasilimali muhimu katika usimamizi na utunzaji wa mazingira nchini. Pamoja na umuhimu huo, vijana wameendelea kuchangia uharibifu wa mazingira katika jitihada za kujitafutia kipato. Changamoto nyingine ni uelewa mdogo miongoni mwa vijana kuhusu umuhimu wa mazingira, mabadiliko ya tabianchi na fursa zinazotokana na uchumi wa buluu; na masuala ya mazingira kutojumuishwa ipasavyo katika programu za maendeleo ya vijana.

**Lengo**
Kuhakikisha ushiriki wa vijana wenye tija katika usimamizi na utunzaji wa mazingira.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:

1.1.1. Kuimarisha mifumo inayowezesha vijana kushiriki na kunufaika na usimamizi na utunzaji wa mazingira;
1.1.2. Kukuza uelewa kuhusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira kwa vijana;
1.1.3. Kuimarisha uwezo wa vijana katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi; na
1.1.4. Kuhakikisha programu za masuala ya vijana zinajumuisha agenda ya usimamizi na utunzaji wa mazingira.

### 3.13. Vijana Wenye Ulemavu

**Maelezo**
Vijana wenye ulemavu wana haki ya kupata fursa za kijamii, kisiasa na kiuchumi kama ilivyoainishwa katika sera, sheria, mikataba na itifaki zinazohusu watu wenye ulemavu.

Hata hivyo, idadi ya vijana wenye ulemavu waliofikiwa na programu za uwezeshaji kijamii, kisiasa na kiuchumi ni ndogo ikilinganishwa na vijana wasiokuwa na ulemavu. Changamoto nyingine ni kuendelea kuwepo kwa mazingira yasiyo rafiki katika baadhi ya maeneo ya mijini na vijijini, hali inayopelekea ushiriki hafifu wa vijana wenye ulemavu katika shughuli za kila siku za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

**Lengo**
Kuimarisha ujumuishwaji wa masuala ya vijana wenye ulemavu katika mipango na programu za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:

1.1.1. Kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa vijana wenye ulemavu katika masuala yote ya kijamii, kisiasa na kiuchumi; na

1.1.2. Kuhakikisha uwepo wa ufikivu wa mazingira, habari, mawasiliano na huduma zingine muhimu kwa vijana wenye ulemavu.

Utekelezaji wenye ufanisi wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007), Toleo la Mwaka 2024 unategemea uwepo wa mfumo wezeshi na madhubuti wa kisheria na kikanuni. Mfumo wa kisheria na kikanuni unaosimamia masuala ya maendeleo ya vijana umejielekeza kwenye sheria mbalimbali ambazo zinapatikana katika sekta na mamlaka mbalimbali zilizoko nchini.

Miongoni mwa sheria na kanuni hizo ni pamoja na Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Sura ya 82; Sheria ya Kitaifa ya Huduma za Ukuzaji Ajira, Sura ya 243; Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366; Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290; na Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348; Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Na.16 ya Mwaka 2004; Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 na Sheria ya Upatikanaji wa Huduma ya Mawasiliano kwa Wote, Sura ya 422. Sheria nyingine ni Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa Kitaifa, Sura ya 193; Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56; Sheria ya Makosa ya Mtandao, Na. 14 ya Mwaka 2015; Sheria ya Vyama vya Kijamii, Sura ya 337; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191, na Sheria ya Watu Wenye Ulemavu, Sura ya 183.

Halikadhalika, uwepo wa sheria hizi umeweka mazingira wezeshi kwa maendeleo ya vijana nchini. Hata hivyo, mifumo ya sheria iliyopo ina dosari zifuatazo:

(i) Kukosekana kwa sheria na kanuni mahsusi zinazolinda na kuimarisha utoaji wa huduma za maendeleo ya vijana;
(ii) Mfumo wa sheria kuwa na wigo mdogo kuwezesha usimamizi na utekelezaji wa masuala ya maendeleo ya vijana; na
(iii) Sheria zilizopo kuwanyima fursa vijana kama kundi la walengwa wakuu wanaohitaji uangalizi maalum na huduma.

Ili kutatua upungufu wa mfumo wa kisheria uliobainika, Serikali itaimarisha utekelezaji wa mifumo ya sheria na kanuni; kufanya mapitio ya sheria na kanuni zilizopo; na kutunga sheria mpya mahsusi zinazolinda na kuimarisha utoaji wa huduma za maendeleo ya vijana nchini.

### 5.1. Mfumo wa Kitaasisi
Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007), Toleo la Mwaka 2024 utafanyika kwa kushirikisha wadau mbalimbali kutokana na ukweli kwamba masuala ya maendeleo ya vijana ni mtambuka. Hivyo, malengo ya sera yatafikiwa kupitia ushirikiano imara wa wadau wakiwemo wizara mbalimbali, sekta binafsi, wadau wa maendeleo ya vijana, asasi za kiraia, taasisi za elimu na utafiti, vijana wenyewe na jamii kwa ujumla.

Vilevile, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007), Toleo la Mwaka 2024 inatambua umuhimu wa uwepo wa sera za sekta nyingine katika kufanikisha malengo yake. Hivyo, utekelezaji wa sera hii utaoanishwa na sera za sekta nyingine pamoja na kuratibu kazi za wadau mbalimbali katika kuendeleza na kuwawezesha vijana nchini.

### 5.2. Majukumu ya Wadau Katika Utekelezaji wa Sera
Utekelezaji wenye tija wa sera hii unategemea uwepo wa mfumo thabiti wa kitaasisi unaoainisha majukumu makuu ya kila taasisi. Wahusika wakuu katika utekelezaji wa sera hii ni pamoja na Wizara Yenye Dhamana ya Maendeleo ya Vijana, Wizara za Kisekta, Idara na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Wadau wengine ni pamoja na wazazi na walezi, vijana, taasisi za dini, washirika wa maendeleo, taasisi za taaluma na utafiti, sekta binafsi, asasi za kiraia na vyombo vya habari.

#### 5.2.1. Wizara Yenye Dhamana na Maendeleo ya Vijana
Wizara hii itasimamia na kuwezesha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007), Toleo la Mwaka 2024. Majukumu mahsusi yatakuwa ni kuratibu na kusimamia utekelezaji wa sera na mipango ya maendeleo ya vijana nchini; kuishauri Serikali kuhusu namna bora ya kuboresha mipango na mikakati kwa maendeleo ya vijana; kutambua na kukuza fursa za uwezeshaji vijana kisiasa na kiuchumi. Majukumu mengine yatakuwa kufanya mapitio ya sera, sheria na miongozo inayohusu maendeleo ya vijana na kuwezesha ujumuishaji wa masuala ya maendeleo ya vijana katika sekta zote.

#### 5.2.2. Wizara Yenye Dhamana ya Masuala ya Fedha
Wizara hii itawezesha upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa programu za maendeleo ya vijana na kuwezesha upatikanaji wa huduma za mikopo nafuu na dhamana kwa vijana. Vilevile, itajumuisha masuala ya maendeleo ya vijana katika mipango, programu, miradi ya maendeleo ya taifa na kutoa vivutio vitakavyowezesha sekta binafsi kustawi na kuzalisha fursa za ajira kwa vijana.

**5.2.3. Wizara Yenye Dhamana ya Masuala ya Mipango na Uwekezaji**
Wizara hii itakuwa na jukumu la kujumuisha masuala ya maendeleo ya vijana katika mipango, programu, miradi ya maendeleo ya taifa na kutoa vivutio vitakavyowezesha sekta binafsi kustawi na kuzalisha fursa za ajira kwa vijana.

**5.2.4. Wizara Yenye Dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**
Wizara hii itaratibu utekelezaji wa sera katika tawala za mikoa na serikali za mitaa; kujumuishwa kwa utekelezaji wa sera katika mipango, mikakati na miongozo ya tawala za mikoa na serikali za mitaa. Pia itakuwa kiungo kati ya sekretarieti za mikoa na wizara yenye dhamana na maendeleo ya vijana kuhusu utekelezaji wa sera ya maendeleo ya vijana.

**5.2.5. Wizara Yenye Dhamana ya Kilimo, Uvuvi na Mifugo**
Wizara hii itakuwa na jukumu la kuwezesha ushiriki na uwekezaji wa vijana katika kilimo, mifugo na uvuvi na kutoa huduma muhimu za ugani na masoko ili kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao mbalimbali yatakayozalishwa na vijana.

**5.2.6. Wizara Yenye Dhamana ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**
Wizara hii itahakikisha mitaala ya elimu na mafunzo ya ufundi inaendana na mahitaji ya soko la ajira; kuweka misingi ya uzalendo, moyo wa kujitolea na utaifa katika mifumo ya elimu; kukuza utoaji wa ujuzi wa kidijitali, ujuzi tepe na ujasiriamali katika mifumo rasmi ya elimu. Aidha, wizara itaanzisha na kuendeleza taaluma ya maendeleo ya vijana katika mifumo rasmi ya elimu na mafunzo ili kuzalisha kada za maafisa vijana wenye ujuzi na umahiri na kuwezesha maendeleo ya uvumbuzi na ubunifu kwa vijana katika ngazi zote.

**5.2.7. Wizara Yenye Dhamana ya Masuala ya Afya**
Wizara hii itakuwa na jukumu la kuimarisha upatikanaji wa huduma rafiki za afya ikiwemo afya ya uzazi kwa vijana; kuimarisha mifumo ya kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya, VVU na UKIMWI, na mimba katika umri mdogo; kuandaa na kutekeleza programu zinazoimarisha afya ya akili na huduma za kisaikolojia kwa vijana. Vilevile, wizara itaimarisha na kutekeleza programu za kuzuia, kudhibiti, utambuzi wa mapema na matibabu ya magonjwa yasiyoambukiza kwa vijana na kuhimiza vijana kushiriki kikamilifu katika uzalishaji, usindikaji na matumizi ya vyakula vyenye lishe ili kudhibiti upungufu wa virutubisho muhimu mwilini.

**5.2.8. Wizara Yenye Dhamana ya Viwanda na Biashara**
Wizara hii itakuwa na jukumu la kuweka mifumo itakayowezesha upatikanaji wa mitaji, masoko, na huduma za ushauri kwa vijana ndani na nje ya nchi; kuhakikisha vijana wanajengewa uwezo wa kumiliki, kusimamia, kuweka akiba, na uendeshaji wa biashara kwenye sekta muhimu za kijamii na kiuchumi.

Pia, wizara itaweka mazingira wezeshi kwa uendelezaji wa biashara zinazoanzishwa na kuendeshwa na vijana na kuboresha mifumo ya urasimishaji wa shughuli za vijana zilizoko kwenye sekta isiyo rasmi.

**5.2.9. Wizara Yenye Dhamana ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**
Wizara hii itakuwa na jukumu la kuandaa na kutekeleza sera, miongozo na mikakati yenye lengo la kuongeza na kuimarisha ushiriki wa vijana katika utamaduni, sanaa na michezo ndani na nje ya nchi.

**5.2.10. Wizara Yenye Dhamana na Usimamizi wa Mazingira**
Wizara hii itakuwa na jukumu la kuandaa na kutekeleza sera, mikakati, mipango na programu zinazowezesha ushiriki wa vijana katika uhifadhi na usimamizi endelevu wa mazingira.

**5.2.11. Wizara Yenye Dhamana ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**
Wizara hii itaendelea kuwajengea vijana wa Kitanzania moyo wa uzalendo, ukakamavu, maadili mema, utaifa na kuwafundisha stadi za kazi; kufungamanisha masuala ya amani na usalama katika programu zote za vijana zinazohusu masuala ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Aidha, wizara itaandaa na kutekeleza programu zitakazowawezesha vijana kushiriki kikamilifu katika shughuli za hiari na za kijamii na kuanzisha na kutekeleza mifumo inayotoa tahadhari mapema ili kuhakikisha vijana wanashiriki ipasavyo katika masuala ya amani na usalama.

**5.2.12. Wizara Yenye Dhamana na Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**
Wizara hii itakuwa na jukumu la kuandaa na kutekeleza sera, mikakati, mipango na programu zinazowezesha ushiriki wa vijana katika sekta ya habari, mawasiliano na teknolojia ya habari.

**5.2.13. Wizara Nyingine za Kisekta, Idara na Wakala za Serikali**
Wizara za kisekta, idara na wakala za serikali zinazojitegemea zitahakikisha malengo ya sera hii yanafungamanishwa katika sera, mikakati, mipango, programu na miradi ya kisekta zinazosimamia na kutekeleza. Pia, zitaanzisha dawati mahsusi kwa ajili ya kusimamia, kutekeleza na kuratibu shughuli zinazohusiana na maendeleo ya vijana.

**5.2.14. Mahakama**
Mahakama itakuwa na jukumu la kutafsiri sheria na kusimamia utoaji wa haki kwa namna ya kukuza uwezeshaji na maendeleo ya vijana.

**5.2.15. Sekretarieti za Mikoa**
Sekretarieti za mikoa zitakuwa na jukumu la kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji, kutoa ushauri wa kitaalamu na kuratibu masuala yote yanayohusiana na maendeleo ya vijana katika mikoa husika.

#### 5.2.16. Mamlaka za Serikali za Mitaa
Mamlaka hizi zitakuwa na jukumu la kutekeleza masuala yote ya maendeleo ya vijana; kujumuisha masuala ya vijana katika sheria ndogo, mikakati, mipango, programu na miradi; kutenga rasilimali na miundombinu kwa ajili ya maendeleo ya vijana, na kuweka mazingira wezeshi kwa wadau mbalimbali kutekeleza masuala ya maendeleo ya vijana.

#### 5.2.17. Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania
Tume itakuwa na jukumu la kutunga sera, mikakati na miongozo ya kukabiliana na VVU na UKIMWI kwa vijana na kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za VVU na UKIMWI zinazohusu vijana.

#### 5.2.18. Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya
Mamlaka itakuwa na jukumu la kuandaa na kutekeleza sera, mikakati na miongozo ya kukabiliana na matumizi ya dawa za kulevya na madhara yake kwa vijana; kuhamasisha vijana kushiriki katika kuzuia matumizi na usafirishaji wa dawa za kulevya, na kufanya tafiti kuhusu masuala yanayohusiana na madawa ya kulevya kwa vijana.

#### 5.2.19. Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira
Baraza itakuwa na jukumu la kuimarisha mifumo inayowezesha vijana kushiriki katika usimamizi na utunzaji wa mazingira; kukuza uelewa kwa vijana kuhusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira; kuimarisha uwezo wa vijana katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha programu za masuala ya vijana zinajumuisha agenda ya usimamizi na utunzaji wa mazingira.

#### 5.2.20. Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi
Baraza litakuwa na jukumu la kuhakikisha mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi vinawafikia na kuwanufaisha kwa usawa vijana waliopo mijini na vijijini.

#### 5.2.21. Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Ofisi hii itakusanya, itatunza na kuhuisha takwimu zinazohusu maendeleo ya vijana kwa ajili ya kuwezesha kupanga, kudhibiti, kutathmini, kuratibu na kutoa maamuzi mbalimbali ya kisera.

#### 5.2.22. Baraza la Vijana
Baraza la Vijana litakuwa ni mojawapo ya majukwaa muhimu katika utekelezaji wa masuala ya vijana ndani na nje ya nchi. Aidha, Baraza litaishauri Serikali kuhusu masuala ya vijana ili kukuza mshikamano kwa vijana bila kujali tofauti za rangi, kabila, jinsi, hali ya kiuchumi, dini, siasa, utamaduni na jiografia.

### 5.2.23. Wazazi na Walezi
Wazazi na walezi watakuwa na jukumu la kuhakikisha vijana wanakuwa na maadili mema, wazalendo na wenye moyo wa kujitolea na utaifa.

### 5.2.24. Familia na Jamii
Familia na jamii watakuwa na wajibu wa kuhakikisha vijana wanakuwa na upendo, uvumilivu, umoja, malezi bora na kuwandaa kuwa raia wema na wawajibikaji.

### 5.2.25. Vijana
Vijana watakuwa na wajibu wa kulinda na kuheshimu tunu za taifa; kuheshimu wazazi, walezi, wazee, wanawake, watoto, watu wenye ulemavu na viongozi; kulinda rasilimali za Taifa. Vilevile, watatakiwa kuwa na moyo wa kujitolea, utaifa na uzalendo, na kutoshiriki katika vitendo vya ukatili, uhalifu na ukandamizaji wa aina yoyote.

### 5.2.26. Asasi za Kiraia
Asasi za Kiraia ni mjumuisho wa Mashirika yasiyo ya kiserikali, asasi za kijamii na asasi za kidini ambazo huchangia katika maendeleo ya vijana hususan katika uwekezaji, utoaji wa huduma, habari na uwezeshaji. Katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007), Toleo la Mwaka 2024 mashirika yatakuwa na jukumu la kuzingatia mfumo wa sheria na kanuni wa maendeleo na uwezeshaji wa vijana; kushiriki katika utoaji wa huduma kwa maendeleo ya vijana na kuandaa taarifa za mara kwa mara za shughuli za maendeleo ya vijana na kuziwasilisha kwa mamlaka zinazohusika.

### 5.2.27. Taasisi za Kitaaluma na Utafiti
Taasisi za kitaaluma na utafiti katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007), Toleo la Mwaka 2024, zitawajibika kuandaa na kuendesha programu maalum zinazohusu maendeleo na uwezeshaji wa vijana na kufanya utafiti na kusambaza matokeo kuhusu masuala  ya maendeleo ya vijana.

### 5.2.28. Vyombo vya Habari
Katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007), Toleo la Mwaka 2024, vyombo vya habari vitakuwa na jukumu la kuelimisha umma kuhusu fursa zilizopo na masuala mengine muhimu ya maendeleo ya vijana na kuwa kiungo muhimu kwa vijana kubadilishana uzoefu katika kutatua changamoto zinazowakabili.

### 5.2.29. Wadau wa Maendeleo
Wadau wa maendeleo watakuwa na jukumu la kutoa misaada ya kitaalamu na fedha kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji na fikiwaji wa malengo ya sera ya maendeleo ya vijana.

## 5.3. Uratibu wa Utekelezaji wa Sera

Mafanikio ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007), Toleo la Mwaka 2024 yanategemea uratibu madhubuti wa wadau wote wanaohusika na masuala ya maendeleo ya vijana nchini. Kwa kuwa utekelezaji wa Sera hii unahusisha wigo mpana wa wadau, uratibu utahusisha wizara, sekta binafsi, washirika wa maendeleo, wakala na wadau wengine.

Katika kufanikisha kazi ya uratibu, Serikali itaandaa na kuweka mifumo thabiti ya kuratibu shughuli zote za maendeleo ya vijana zinazotekelezwa na wizara, idara na mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali. Mifumo hiyo ni pamoja na kuunda kamati na kikosi kazi cha wataalam ya kitaifa wa masuala ya maendeleo ya vijana.

## 5.4. Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini

Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utatumika kupima kiwango kilichofikiwa cha utekelezaji wa malengo mahsusi ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007), Toleo la Mwaka 2024. Utekelezaji wenye tija wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini unategemea uratibu na utendaji kazi wa vipengele vyote vya mfumo kuanzia ukusanyaji wa takwimu, uchambuzi na utoaji taarifa kwa wadau. Mfumo huo unahusisha uandaaji na utoaji wa taarifa kuhusu hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa sera.

Wizara yenye dhamana ya maendeleo ya vijana itaratibu, fuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (20070, Toleo la Mwaka 2024 kwa kushirikiana na wadau wakuu wakiwemo wizara za kisekta, idara na wakala za serikali zinazojitegemea, sekretarieti za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa, mahakama, bunge, sekta binafsi, vyombo vya habari, mashirika yasiyo ya kiserikali na wadau wa maendeleo. Katika kuhakikisha mfumo huu unakuwa na ufanisi, kila mdau atalazimika kuwa na mfumo wa ndani wa ufuatiliaji na tathmini ambao pamoja na mambo mengne utahakikisha unatathmini ufanisi wao katika kutekeleza sera.

Vilevile, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utahusisha kufanya tathmini ya msingi na kuweka viashiria vya upimaji. Aidha, kutakuwa na mapitio ya kila mwaka, ambayo yatajielekeza kutathmini iwapo shughuli zilizopangwa zinaendana na malengo yaliyowekwa. Halikadhalika, mapitio hayo yatahusisha kufanya tafiti mbalimbali ili kupata mrejesho wa matokeo yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa sera.

## 5.5. Hitimisho

Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007), Toleo la Mwaka 2024 ni mwongozo wa kisera wa Serikali katika kuendeleza na kuboresha hali ya maisha na ustawi wa vijana nchini. Sera inamtambua kijana kama mtu yeyote wa kike au kiume mwenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi 35. Katika umri huo, vijana wanategemewa kushiriki kikamilifu katika shughuli zote halali kwa hiari ili kuchangia maendeleo ya Taifa. Sera hii ina lengo la kutoa mwongozo kwa wadau wa maendeleo ya vijana katika uwezeshaji na ushiriki wa vijana kwenye shughuli za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Sera hii inazingatia masuala mbalimbali yanayohusu vijana ikiwa ni pamoja na elimu, ajira, afya, malezi na maadili, kilimo, michezo, utamaduni na ushiriki wa kisiasa. Aidha, utekelezaji wa masuala haya ya kisera, utawezesha Taifa kuwa na vijana wenye ujuzi, ubunifu, ufahamu na matumizi sahihi ya teknolojia, waliowezeshwa na kulelewa vyema, wazalendo na wawajibikaji.

Ofisi ya Waziri Mkuu,
Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu
Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Kazi,
S.L.P 2890.
40411 DODOMA, TANZANIA.
Simu: 026 2963450/51
Barua pepe: ps@kazi.go.tz
Tovuti www.kazi.go.tz